# Uelekeo

*Leo yetu ndiyo kesho yetu*




Yanga kurejea mahala pake leo?

| ISSN 2953-2787 | Toleo Na. 00030 | Bei Tanzania sh 1,000 | Jumatano Septemba 20 - 26, 2023 |

# Samia aandika historia Kilwa

- **Asema isipobadilika, viongozi wajiulize kunani**

Uk. 4



Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, akiwa na Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega, Mkuu wa Mkoa wa Lindi, Zainab Telack, Waziri wa Tamisemi, Mohamed Mchengerwa na viongozi wengine wakati akikata utepe kuzindua ugawaji wa boti za uvuvi 34 za mkopo nafuu mara baada ya kuweka jiwe la msingi ujenzi wa Bandari ya Uvuvi, Kilwa Masoko mkoani Lindi jana.

## ...azidi kufungua milango ya uwekezaji

Kwa miaka mingi uhusiano wa kibiashara baina ya nchi mbili hizi, umekuwa ukiongezeka kwa kasi kubwa ambapo wafanyabiashara baina ya mataifa haya wamekuwa wakifanya biashara yenye thamani kubwa.

Uk. 4



## Wizara ya Afya kufanya tathmini ya Uviko-19

Uk. 3

## 'Umeme ufike hapa haraka'

**Na Mwandishi Wetu, Songea**


WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge na Uratibu), Jenista Mhagama, ameliagiza Shirika la Umeme Tanzania (Tanesco) kupitia Wakala wa Nishati Vijijini (REA), kuhakikisha linafikisha huduma ya umeme katika Kijiji cha Ngahokora ifikapo Desemba, mwaka huu.

Inaendelea Uk. 2




## Kasi utengenezaji mabehewa treni mwendokasi

Uk. 8



## Hatuna sababu kuagiza matufaa nje

Uk. 14



## NIPELEKENI NIPIGE KURA




**Kikongwe akisaidiwa kwenda kupiga kura kutimiza haki yake ya Kikatiba ya kumchagua kiongozi amtakaye katika kituo cha kupigia kura cha Kata ya Mfaranyaki, Halmashauri ya Manispaa ya Songea mkoani Ruvuma jana.**

**Picha: (Mpigapicha Wetu)**

# MNH yafanikiwa upasuaji wa tundu dogo moja

**Na Mwandishi Wetu**

HOSPITALI ya Taifa Muhimbili (MNH), imefanikiwa kufanya upasuaji wa kwanza wa kifua kwa mgonjwa ili kuondoa uvimbe kwenye pafu kutumia tundu dogo moja.

Upasuaji huo uliwashirikisha watalaamu wazalendo ukiongozwa na Bingwa wa Upasuaji Kifua Duniani na mgunduzi wa upasuaji wa aina hiyo, Dk. Diego Gonzalez Rivas kutoka nchini Hispania.

Mkurugenzi wa Huduma za Upasuaji (MNH) Dk. Rachel Mhaville, alisema upasuaji huo ni mwendelezo wa azma ya serikali kuhakikisha huduma za kibingwa na ubingwa bobezi, zinatolewa nchini na kuleta unafuu kwa wananchi na serikali kwa ujumla ambao pia unaifanya Tanzania kuwa nchi ya kwanza kutumia tundu moja dogo kupitia hospitali ya umma katika Ukanda wa Afrika Mashariki na Kati ukilinganisha na matundu matatu yaliyozoeleka sehemu nyingine duniani.

Mkuu wa Idara ya Upasuaji MNH, Dk. Ibrahim Mkoma, alisema mgonjwa akifanyiwa upasuaji huo ambao siyo wa kufungua kifua, anaweza asihitaji kukaa ICU kama wagonjwa wengine wa upasuaji wa kawaida na akaruhusiwa siku ya pili au ya tatu yake na kuendelea shughuli zake za kawaida.

Dk. Mkoma alisema wagonjwa wapatao wanne wanategemewa kufanyiwa upasuaji wa aina hiyo na mara baada ya hapo, watalaamu wazalendo wataendelea kutoa huduma hiyo kwa wananchi wenye changamoto mbalimbali.

# Mambo mazuri reli ya kisasa

**Na Mwandishi Wetu, Mwanza**

BODI ya Wakurugenzi wa Shirika la Reli Tanzania (TRC), imemaliza ziara ya kukagua mradi wa ujenzi wa reli ya kisasa (SGR), kipande cha tano kinachotoka Isaka hadi Mwanza na kuridhishwa na namna kasi ya ujenzi unavyoendelea.

Akizungumza wakati wa ziara hiyo jana, Meneja Mradi Msaidizi wa k

Kituo cha Mwanza -Isaka, Moga Kulwa, alisema ujenzi wa mradi huo umefikia asilimia 39.

Alisema katika kipande cha tano cha Mwanza-Isaka kutakuwa na jengo la abiria, ambalo litakuwa na uwezo wa kuhudumia abiria 961 kwa wakati mmoja.

"Mpaka sasa mradi wetu tunategemea ukamilike mwaka 2024 mwezi wa Mei na kwa kweli mradi huu utawasaidia sana wananchi hususani wafanyabiashara kwa sababu usafiri huu utakuwa unatumia saa nane tu kutoka Mwanza hadi Dar es Salaam na usafiri utakuwa wa bei nafuu," alisema Kulwa.

Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi wa TRC, Ally Karavana alisema mradi unaendelea vizuri na hivyo Watanzania watarajie kwamba mradi utakamilika kwa wakati.

Naye Kaimu Mkurugenzi wa TRC, Amina Lumuli alisema lengo la ziara hiyo ni kuipa uelewa bodi mpya ya wakurugenzi kuhusu mradi wa SGR.

# 'Fikisheni umeme hapa haraka'

**Inatoka Uk. 1**

Waziri Mhagama alitoa agizo hilo jana baada ya kuzindua madarasa ya mfano ya Elimu ya Awali katika Shule ya Msingi Ngahokora, iliyopo Kata ya Kizuka, Kijiji cha Ngahokora, Songea Vijijini ikiwa ni mwendelezo wa ziara yake katika Jimbo la Peramiho mkoani Ruvuma.

Waziri Mhagama alisema kufikishwa kwa huduma hiyo muhimu itakuwa mkombozi kwa wakazi wa eneo hilo katika kujikwamua kiuchumi.

Alifafanua kwamba umeme utawasaidia wananchi katika shughuli za uzalishaji na mali na matumizi ya nyumbani pamoja na huduma za afya pale wananchi wanapokwenda kupatiwa matibabu katika zahanati na vituo vya afya.

"Ilani ya Chama Cha Mapundizi (CCM) tunaitekeleza kwa miaka mitano na sasa tunamalizia mwaka wa tatu umeme umefika Magagula kisha ukaelekea Kizuka na mwaka 2023 umeme utaelekea Mbilo na kisha hapa Ngahokora kwa sababu kama serikali tunatambua umuhimu wa nishati hii muhimu katika maendeleo kuanzia ngazi ya familia na Taifa," alisema.

Aidha, alimpongeza Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, kwa kuendelea kuboresha huduma za afya kwa kujenga Hospitali ya Wilaya iliyopo Mpitimbi na kwamba zaidi ya Sh. bilioni mbili, zimetumika katika ujenzi wa hospitali hiyo na kutoa wito kwa wananchi kuitumia kupata huduma.

"Wakazi wa Ngahokora ninyi ni, sehemu ya wanufaika wa ile hospitali ya Wilaya ya Mpitimbi ambayo zaidi ya Sh. bilioni mbili zimetumika pale. Hiyo itawasaidia msitembee umbali mrefu kutafuta matibabu kutoka hapa Ngahokora na ni rahisi kufika hospitalini hapo kuliko kwenda Peramiho," alisisitiza Waziri Mhagama.

Naye Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Songea, Menas Komba, alisema kijiji hicho kilikuwa kinakabiliwa na changamoto mbalimbali zikiwemo barabara, maji, uhaba wa vitanda vya kujifungulia kwa kina mama, umeme pamoja na mawasiliano lakini serikali imeendelea kuzitatua kuhakikisha wananchi wanapata huduma muhimu na kufanya shughuli za uzalishaji.

Kwa upande wake, Diwani wa Kata ya Kizuka, Jacob Nditi, alisema utekelezwaji wa miradi mikubwa ya maendeleo inayofanywa na serikali katika kijiji hicho inaonesha nia njema ya serikali ya awamu ya sita ya kuwaletea wananchi wake maendeleo na mabadiliko ya kiuchumi.

Ofisa Mtendaji wa Kijiji cha Ngahokora, Tumaini Kaaya, aliishukuru serikali kwa kuendelea kuboresha miundombinu ya elimu akisema kuwa kukamilika kwa madarasa kutatoa mwamko kwa wazazi kupeleka watoto shule na wanafunzi watakua kwenye mazingira mazuri ya kujifunza.

# Wizara ya Afya kufanya tathmini ya Uviko-19

**Na Emmy Jovin**

WIZARA ya Afya, imeanza kufanya tathmini kubaini changamoto na mapungufu katika mapambano dhidi ya ugonjwa wa Uviko-19 na namna Tanzania ilivyokabiliana na mlipuko wa ugonjwa huo.

Mfamasia Mkuu wa Serikali, Daud Msasi, alisema hayo jijini Dar es Salaam juzi kwa niaba ya Katibu Mkuu wa Wizara ya Afya wakati akifungua kikao cha kwanza kwa ajili ya kufanya tathmini hiyo.

Alisema lengo la kikao hicho ilikuwa ni kuanisha masuala yaliyofanyika vizuri na kubaini changamoto na mapungufu katika mapambano ya mlipuko wa ugonjwa huo.

Aliwataka washiriki wote katika kikao hicho kuwa huru kutoa taarifa na maoni yao kwa kuwa kikao hicho hakina lengo la kumlaumu mtu isipokuwa kimelenga zaidi kufanya tathmini na kuboresha njia nzuri za kukabiliana na magonjwa au majanga pindi yatakapojitokeza tena.

Kwa upande wake, Kaimu Mkurugenzi wa Huduma za Dharura na Maafa katika Wizara ya Afya, Angela Samwel alisema taarifa ya tathmini hiyo itahusisha masuala mazuri yaliyofanywa wakati wa kukabiliana na Uviko-19, changamoto zilizojitokeza, mapungufu yaliyokuwepo na kupendekeza hatua za muda za kuboresha mapungufu yaliyojitokeza.

Alisema ripoti ya utafiti huo itawasilishwa kwa viongozi na wadau mbalimbali.

Alisema ugonjwa wa Uviko-19 umeendelea kutolewa taarifa duniani kote na kwa sasa umeonekana kupungua kwa kiasi kikubwa hivyo kusababisha baadhi ya masharti yaliyowekwa kupungua katika maeneo mengi.

Shirika la Afya Duniani (WHO) limetoa tamko kuwa ugonjwa huo siyo wa dharura ya kiafya kimataifa.



**Balozi wa Marekani nchini Dk. Michael Battle akitoa cheti kwa mshiriki kati ya wanawake 30 kutoka Pemba, jana waliopatiwa mafunzo maalumu ya wiki 13 katika biashara na ujasiriamali yaliyofadhiliwa na Serikali yaMarekani kupitia kupitia programu yake ya kuwajengea uwezo wajasiriamali wanawake(Academy of Women Entrepreneurs – AWE).**

# Wanawake 30 wahitimu mafunzo ya ujasiriamali

**Na Mwandishi Wetu**

WANAWAKE 30 wanaojishughulisha na ujasiriamali kutoka Pemba, jana walihitimisha mafunzo maalumu ya wiki 13 katika kuboresha biashara na ujasiriamali.

Mafunzo hayo yalifadhiliwa na Serikali ya Marekani kupitia programu yake ya kuwajengea uwezo wajasiriamali wanawake (Academy of Women Entrepreneurs – AWE).

Akizungumza wakati wa kufunga mafunzo hayo, Balozi wa Marekani nchini, Dk. Michael Battle aliwapongeza wanawake hao akiwahimiza kutumia mafunzo waliyoyapata kuendelea kujenga biashara zenye tija na mafanikio.

"Mafunzo mliyoyapata mkiwa sehemu ya programu hii yamewapa ujuzi kwa vitendo utakaowawezesha kuanzisha biashara endelevu pamoja na kuwaunganisha na wakufunzi (mentors) na wajasiriamali wengine kama ninyi wa nchini Marekani," alisema.

Alisema kuwajengea wanawake uwezo wa kiuchumi ndio njia ya haraka zaidi ya kuibadilisha jamii.

"Jitihada za wanawake huwa na matokeo makubwa zaidi kwa jamii nzima kwa sababu wanawake wanapofanikiwa mara nyingi huwekeza mapato yao katika familia na jamii zao, wakigharamia mahitaji kama vile ada kwa watoto wao na huduma za afya. Manufaa ya kiuchumi ya mafanikio yenu yanasaidia vizazi vijavyo," alisema.

Hafla hiyo pia ilihudhuriwa na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji wa Zanzibar, Mudrick Ramadhan Soraga na Mkuu wa Mkoa wa Kusini Pemba, Salama Mbarouk Khatib.

Wengine waliohudhuria ni Mkuu wa Wilaya ya Chake Chake, Abdalla Rashid Ali, Mratibu wa Maktaba ya Taifa Pemba, Ahmed Amour na wageni wengine waalikwa.

AWE ni mpango wa Kimataifa wa Serikali ya Marekani unaokusudia kuwajengea uwezo wa kiuchumi wanawake milioni 50 duniani kote.

Kundi la wahitimu wa Pemba ni la kumi la washiriki wa programu ya AWE. Makundi mengine ya wanawake walioshiriki katika programu hiyo ni kutoka Dar es Salaam, Iringa, Zanzibar, Mwanza, Dodoma, Mbeya, Bagamoyo, Kigoma na Kagera. Kupitia Ubia na Taasisi ya Marekani ya Maendeleo ya Afrika (U.S. African Development Foundation - USADF), wajasiriamali wanaoshiriki programu ya AWE wanaweza kupatiwa fedha za mtaji wa hadi Dola za Marekani 20,000 ili kupanua biashara zao.

Ubalozi wa Marekani unashirikiana na taasisi ya Selfina kutekeleza programu ya AWE nchini.

# Mavunde agawa vifaa vya maabara shuleni

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI wa Madini na Mbunge wa Dodoma Mjini, Anthony Mavunde, amegawa vifaa vya maabara vyenye thamani ya Sh. mililioni tisa kwa ajili ya masomo ya sayansi kwa shule za sekondari.

Katika hafla ya ugawaji wa vifaa hivyo iliyofanyika Shule ya Sekondari Wella iliyopo Kata ya Kikuyu Kusini katika Halmashauri ya Jiji la Dodoma, juzi,

Mavunde aliwahamasisha wanafunzi kuwa elimu ni mkombozi na itawasazidia kuinua maisha yao na kuleta maendeleo kwa Taifa.

"Ninaamini elimu ni mkombozi wa kweli kwa vijana kwani itawasaidia kutoa mchango wa kulitumikia Taifa na familia zenu.

"Nilipobaini tunachangamoto ya vifaa katika maabara zetu nyingi, niliamua nianze na awamu ya kwanza na hii haitakuwa mwisho, nitajitahidi kuzifikia maabara nyingine zaidi."

"Leo nimeanza na shule tatu na mzigo huu wa kwanza umenigharimu Sh. milioni tisa na nitaendelea kufanya hivi kwa sababu dhamira yangu ni kuhakikisha wanafunzi wetu wanafanya vizuri," alisema.

Akielezea mikakati yake kwa Halmashauri ya Jiji la Dodoma alisema ni kukuza elimu.

"Mkakati wa kwanza nilionao ni kukuza elimu mkoani hapa hasa Jimbo la Dodoma Mjini. Nimesikia changamoto ya walimu wa sayansi, hii ni changamoto kubwa na mimi suluhisho ninalo na nimeshaanza kulifanyia kazi.

# Samia aandika historia Kilwa

## ● Asema isipobadilika, viongozi wajiulize kunani




Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, akiwa na Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega, wakati akitoa mfano wa funguo kwa Shukrani Shamte na Juma Omari Juma, kama ishara ya kugawa boti 34 za mkopo nafuu kwa vikundi vya uvuvi baada ya kuweka jiwe la msingi ujenzi wa Bandari ya Uvuvi iliyopo Kilwa Masoko mkoani Lindi jana.



**Mwandishi Wetu na Shamila Mkomweke TURDAco**

RAIS Dk. Samia Suluhu Hassan, ameandika tukio kubwa la kihistoria kwa kuzindua ujenzi wa mradi wa Bandari ya Uvuvi ya kisasa, Inayojengwa Kilwa Masoko mkoani Lindi.

Tukio hilo lilikwenda sambamba na ugawaji wa boti 160 za kisasa kwa ajili ya vikundi vya wavuvi na wanawake wanaojishughulisha na kilimo cha mwani.

Kuhusu bandari hiyo ya kwanza ya aina yake nchini, Rais alisema mradi huo hadi utakapokamilika utagharimu Sh. bilioni 266, fedha za ndani. Mradi unatarajiwa kuchukua miaka mitatu.

Akiweka jiwe la msingi la ujenzi wa bandari hiyo, akiwa katika ziara yake mkoani Lindi jana, Rais Dk. Samia aliwataka wananchi wa Kilwa kubadilika na kutumia miradi hiyo kwa maendeleo yao na taifa kwa jumla.

Alisema wanafikiria kujenga bandari nyingine ya uvuvi Bagamoyo mkoani Pwani pale hali ya uchumi itakaporuhusu.

"Leo tumeweka jiwe la msingi kwa mradi huu mkubwa sana… Kubwa lao katika Mkoa wa Lindi na Tanzania kwa ujumla. Hii ni bandari ya kwanza (ya uvuvi) kujengwa nchini," alisema.

"Fedha zilizoingia Kilwa ni nyingi sana kwa ajili ya maendeleo, tumemimina fedha nyingi katika elimu, afya, umeme, barabara na kadhlika, sasa tunataka Kilwa ibadilike na isipobadilika mjiulize kwa nini.

"Fedha zimeletwa ili ziwaondoleeni dhiki na siyo viongozi wajinufaishe. Kilwa isipobadilika, viongozi wajiulize kuna tatizo gani hapo?" Alisema.

Akizindua ugawaji wa boti 160 za kisasa, Dk. Samia alisema boti hizo kwa upande wa uvuvi zina uwezo wa kuona samaki walipo baharini na kila moja ina wezo wa kuhifadhi tani moja ya samaki wabichi waliogandishwa hadi watakapofikishwa ufukweni kwa ajili ya kuchakatwa.

Kwa upande wa wakulima alisema boti hizo zitarahisisha kazi ya kupanda mwani hadi maeneo ya kina kirefu baharini na ubebaji wa mwani kiasi cha tani moja kwa wakati mmoja.

Uzinduzi wa ugawaji wa boti hizo kwa awamu ya kwanza ulihusisha boti 34 ambazo kati yake, 21 zilikwenda kwa vikundi vya wanawake wanaojihusisha na kilimo cha mwani.

Rais Samia alisema boti hizo zimetolewa na Serikali kwa mkopo nafuu usio na riba, na hivyo akawakata wanufaika kuweka utaratibu mzuri wa kurejesha mkopo huo.

Aidha alisema Kilwa ipo katika mazingira mazuri ya kuendelea kutokana na biashara ya uvuvi na ufugaji wa samaki hususani, katika maeneo ya mikoko na maeneo ya mito yanayoingiza maji baharini.

"Mkiamua kufuga samaki kwenye mikoko na mito, Kilwa itabadilika sana…

Serikali itapeleka wataalamu kusaidiana na wafugaji hao.

"Tunapenda kuinua hali yenu ya kiuchumi na hatutarajii boti hizi ziwe chanzo cha migogoro katika vikundi vyenu. Matarajio yetu ni kwamba miaka miwili hadi mitatu hivi ijayo, Kilwa lazima ibadilike kwa kupiga hatua kubwa ya maendeleo na isipobadilika lazime mjiulize kwa nini," alirdua kusisitiza.

Katika hatua nyingine, Rais Dk. Samia aliwaonya wavuvi dhidi ya matumizi ya baruti katika shughuli za uvuvi akisema yanaharibu matumbawe ambayo ni maeneo ya mazalio ya samaki.

Mapema, Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega alimpongeza Rais Samia kwa ujenzi wa Bandari ya Uvuvi ya Kilwa Masoko, ambayo itakwenda kutoa ajira kwa vijana takribani 30,000 kutoka maeneo mbalimbali nchini.

Alisema bandari hiyo itasaidia kukua kwa soko kubwa la samaki ambalo pia litategemewa na mataifa ya jirani kwa kuwa na uwezo wa kuhifadhi kwa wakati mmoja tani 1,300 za samaki waliogandishwa.

Alisema bandari hiyo itakuwa na karakana ya kutengeneza meli, sehemu ya kusimama meli kubwa zisizopungua 10 na karakana ya kutengeneza nyavu kwa ajili ya shughuli za uvuvi.

## ...azidi kufungua milango ya uwekezaji

RAIS Samia Suluhu Hassan, ameendelea kufungua milango ya uchumi ya kibiashara ambapo wawakilishi wa kampuni 30 kutoka Uturuki, wako nchini kutafuta fursa mbalimbali za uwekezaji na ubia na wawekezaji Watanzania.

Ujumbe huo wa wafanyabiashara ulikutana na wenzao wa Tanzania kutoka kampuni 100 na wawakilishi wa asasi mbalimbali za kibiashara.

Baadhi ya taasisi zilizoshiriki mkutano huo ni Chemba ya Biashara, Viwanda na Kilimo (TCCIA), Shirikisho la Wenye Viwanda na Biashara (CTI), Taasisi ya Sekta Binafsi Tanzania (TPSF) na Chemba ya Wafanyabiashara Wanawake Tanzania (TWCC).

Mkutano huo ulifunguliwa jana na Waziri wa Viwanda na Biashara, Dk. Ashatu Kijaji na Balozi wa Uturuki nchini, Dk. Mehmet Gulluoglu.

Akizungumza wakati akifungua mkutano huo, Waziri Kijaji alisema Tanzania na Uturuki zimekuwa na uhusiano mzuri wa kibiashara katika sekta mbalimbali.

"Kwa miaka mingi uhusiano wa kibiashara baina ya nchi mbili hizi, umekuwa ukiongezeka kwa kasi kubwa ambapo wafanyabiashara baina ya mataifa haya wamekuwa wakifanya biashara yenye thamani kubwa," alisema

Alisema hata ndege za Uturuki, zimekuwa zikifanya safari za moja kwa moja kutoka Instambul nchini Uturuki kuja moja kwa moja Dar es Salaam mara tatu kwa wiki.

Waziri Kijaji alisema safari hizo za ndege kwa kiwango kikubwa, zimesaidia kufungua utalii na biashara mbalimbali baina ya mataifa hayo mawili.

Alisema kwa miaka 26 sasa bidhaa zinazoingizwa nchini kutoka Uturuki, zimeongezeka kwa asilimia 17.3, kutoka Dola za Marekani milioni 4.55 mwaka 1995 na kufikia Dola za Marekani milioni 500 milioni mwaka 2022.

Alisema mwaka 2021, Tanzania iliuza bidhaa zenye thamani ya Dola za Marekani milioni 37.6 nchini Uturuki na bidhaa kubwa ilikuwa dhahabu ambayo ilikuwa Dola milioni 14.9 na tumbaku ghafi Dola za Marekani milioni 11.2.

"Natumaini ujumbe huu wa wafanyabiashara, utaongeza chachu ya biashara kwa kutumia fursa mbalimbali zinazopatikana kwenye mataifa haya mawili na kwa sasa kuna kampuni kubwa ya Uturuki ya Yapı Merkezi, ambayo inajenga mradi wa thamani ya Dola bilioni 3.1," alisema Waziri Kijaji.

Alisema mradi huo ni mkubwa kuwahi kutokea kwenye historia ya Tanzania na kwamba kukamilika kwake kutaingunisha Tanzania na nchi za Burundi, Rwanda na Congo DRC kwa kuwa na treni ya kisasa.

Balozi wa Uturuki nchini, Gulluoglu, alisema wafanyabiashara kutoka kampuni hizo wanatoka sekta mbalimbali zikiwemo teknolojia, ujenzi na utengenezaji wa nguo.

"Tumekuja kukutana na wafanyabiashara zaidi ya kampuni 100 za Tanzania kubadilishana mawazo na namna tunavyoweza kufanya biashara pamoja tunashukuru mkutano umekwenda vizuri," alisema.

Alisema mafanikio ya mkutano huo yametokana na uhusiano mzuri baina ya Serikali za Uturuki na Tanzania ambazo zimekuwa zikifanya biashara za thamani kubwa ya fedha.

"Tanzania na Utururi hatushindani kibiashara, bali ni washirika ambao tumekuwa tukisaidiana kwenye kuimarisha biashara mbalimbali kwa Watanzania kupeleka bidhaa Uturuki na Uturuki kuleta bidhaa hapa Tanzania," alisema.

# Ziara ya Rais Samia Mikoa ya Lindi, Mtwara




















# Maoni ya Mhariri & Uchambuzi

## HII NI KERO

### Kutumikisha watoto katika utafutaji pesa

KUNA tabia ya baadhi ya wazazi na walezi, wenye tabia ya kuwatumikisha watoto wadogo (wanafunzi) majukumu ya kutafuta pesa badala ya kuwahimiza kwenda shule.

Idadi ya watoto wenye umri wa kwenda shule wanaoonekana mitaani mudsa wa masomo wakifanya biashara ya kutembeza/kuuza matunda, mbogamboga, vitafunwa na bidhaa nyingine imekuwa ikiongezeka.

Ushauri wangu kwa wazazi/walezi kama hao wawaache watoto wasome kwa sababu elimu ni ufunguo wa maisha. Elimu itawawezesha watoto kuwa viongozi, wafanyabiashara na wajasiriamali wa kesho na hivyo kujenga familia bora na Taifa lenye uchumi imara.




## MAONI YA MHARIRI

# Boti 'za Samia' zinufaishe Taifa

JANA, Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, alizindua ugawaji wa boti 160 za kisasa kwa wananchi wa Wilaya ya Kilwa ili ziwasadie katika shughuli zao za uvuvi na kilimo cha zao la mwani.

Boti hizo za uvuvi, zina uwezo wa kuona samaki walipo baharini na kila moja ina wezo wa kuhifadhi tani moja ya samaki wabichi waliogandishwa hadi watakapofikishwa ufukweni tayari kwa kuchakatwa.

Kadhalika, kwa upande wa wakulima, boti hizo zitarahisisha kazi ya kupanda mwani hadi maeneo ya kina kirefu baharini na ubebaji wa mwani kiasi cha tani moja kwa wakati mmoja.

Uzinduzi wa ugawaji wa boti hizo kwa awamu ya kwanza ulihusisha boti 34 ambazo kati yake, 21 zilikwenda kwa vikundi vya wanawake wanaojihusisha na kilimo cha mwani.

Rais Dk. Samia aliwaeleza wananchi wa Kilwa kuwa boti hizo zimetolewa na serikali kwa mkopo nafuu usio na riba, na hivyo kuwataka wanufaika kuweka utaratibu mzuri wa kurejesha mkopo huo.

Alisema Kilwa ipo katika mazingira mazuri ya kuendelea kutokana na biashara ya uvuvi na ufugaji wa samaki hususani, katika maeneo ya mikoko na maeneo ya mito yanayoingiza maji baharini.

UELEKEO kwanza tunampongeza Rais Dk. Samia kwa hatua hiyo ambayo hakika imelenga kuwakomboa wananchi wa Kilwa, Mkoa wa Lindi na Tanzania kwa jumla.

Jambo la msingi ambalo Rais alisisitiza nasi UELEKEO tunaliunga mkono, ni kwamba, boti hizo zisijekuwa chanzo cha wananchi kuvurugana na kukosa kuelewana.

Lengo la serikali kugawa boti hizo, ni kutaka wananchi wake wajipatie kipato kupitia uvuvi na kilimo.

Haitakuwa na maana badala ya kuzitumia kwa lengo lililokusudiwa, zikageuka kujenga uhasama na uadui miongoni mwa wananchi.

Tuna uhakika kwamba, viongozi wa Mkoa wa Lindi kwa ujumla wao, watasimamia kwa haki ili boti hizo zigawiwe kwa usawa na bila upendeleo wowote kulingana na mahitaji halisi.

Jambo la kufurahisa zaidi ni kwamba Rais Samia aliahidi kwamba serikali itapeleka wataalamu kusaidiana na wafugaji hao.

Aidha, alisisitiza kuwa ni matarajio ya serikali kuwa boti hizo zitainua hali ya kiuchumi ya wananchi.

Ni matarajio ya gazeti hili kwamba ndani ya miaka miwili hadi mitatu ijayo kama alivyosema Rais Dk. Samia, Kilwa itabadilika kwa kupiga hatua kubwa ya maendeleo kutokana na matumizi bora ya boti hizo.

## Wasiliana nasi

| | |
|---|---|
| **Mhariri Mkuu:** +255713263775 / +255748115000 | **S. L. P:** 15110, Dar es Salaam |
| **Mhariri wa Habari:** +255753333330 | **Makao Makuu Mtaa:** Barabara ya Morogoro |
| **Mhariri Michezo:** +255787559090 | **Jengo la:** Aura Mall |
| **Meneja Masoko/Biashara:** + 255718480406 / + 255733768825 | **Chumba Cha Habari:** +255 (0)222151532 |
| | **Email:** uelekeohabari@gmail.com |



Na Godfrey Sanga
JICHO LANGU
Sangagodfrey26@gmail.com

# Umoja wetu ndiyo amani yetu

TANZANIA ni nchi yenye mfumo wa vyama vingi vya siasa uliorejeshwa katika Katiba ya Tanzania, mwaka 1992.

Mfumo wa vyama vingi ni hali ya kuwa na chama zaidi ya kimoja katika nchi moja. Madhumuni ya kuwa na vyama vingi vya siasa ni kuleta ushindani wa kisiasa ili kuleta maendeleo ya nchi.

Ukweli ni kwamba upinzani wa kisiasa sio uadui kama watu wengi kwenye nchi zinazoendelea wanavyofikiri au kudhani. Kuwa na vyama vingi ni kuongeza wigo wa demokrasia katika jamii husika.

Moja ya manufaa ya vyama vingi ni kukosoa na kuisaidia serikali kufanya vizuri zaidi katika uendeshaji wa nchi, kupanua wigo wa majukwaa ya kidemokrasia na uhuru wa kuchagua, kushiriki masuala ya siasa za nchi, kushiriki harakati za maendeleo kila ngazi kuanzia kitongoji, kijiji, kata, tarafa, wilaya, kanda, hadi Taifa.

Pia huchochea serikali kusukuma maendeleo kwenye majimbo au halmashauri zinazoongozwa na upinzani ili kupata ushawishi zaidi katika chaguzi zinazofuata na kuimarisha siasa za ushindani miongoni mwa wananchi, wanasiasa na viongozi.

Septemba 11 mwaka huu, Rais Dk. Samia Suluhu Hassan alikutana na Baraza la Vyama vya Siasa nchini, katika mkutano maalumu na wadau wa demokrasia ili kutathimini utekelezaji wa mapendekezo ya Kikosi kazi kilichoteuliwa na Rais kuhusu hali ya siasa nchini.

Katika kuonesha uwepo wa ushirikiano na kuelewana baina ya chama kimoja na vyama vingine, wawakilishi kutoka vyama mbalimbali walikutana jijini Dar es Salaam kusikiliza, kujadili na kutoa mapendekezo mbalimbali.

Tanzania ni nchi ya mfano kwa amani, utulivu pamoja na ushirikiano baina ya mtu mmoja na mwingine chini ya mwavuli wa vyama vingi vya siasa, hii ni tofauti na mataifa mengine ambayo mara kwa mara yamekuwa na mapigano kwa sababu ya tofauti ya vyama vyao vya siasa.

Licha ya viongozi wengi wa Taifa hili waliowahi kupita katika nafasi zao za utawala kusisitiza kuondokana na tofauti zetu za itikadi, lakini katika mkutano huo Rais Samia alisikika akisisitiza kuwa Tanzania yetu ni moja na tuna haki ya kujivunia tunu ya amani tuliyonayo.

> **Tanzania ni nchi ya mfano kwa amani, utulivu pamoja na ushirikiano baina ya mtu mmoja na mwingine chini ya mwavuli wa vyama vingi vya siasa**

Aidha, Rais Samia alikemea matumizi mabaya ya majukwaa ya siasa ikiwemo kubeza utu wa mtu, kuibua taharuki kwa wananchi na kauli za kichochezi, badala ya kutumia fursa hiyo kunadi sera kwa wananchi ili kujiimarisha kuelekea chaguzi za 2024 na 2025.

"Tumeruhusu mikutano ya hadhara ili vyama vya siasa vizungumze…, hatukutoa fursa ile kutukana, kukashifu dini za watu ila najua kwanini haya yanatokea, ni kwakuwa cha kuongea hakuna," alisisitiza Rais Samia kuwa na majukwaa ya kizalendo.

Jicho langu linatambua na linaona mengi makubwa, linaona Tanzania yenye upendo, utulivu na mafanikio endapo kila mmoja akiheshimu itikadi za mwingine kupitia chama chake.

Ushauri wangu kwako wewe kiongozi wa siasa na wanasiasa kuwa hakuna Tanzania nyingine baada ya vita, umoja wetu ndiyo amani yetu.

Kazi Iendelee

# Kituo kipya cha Afya Tygelo kuhudumia wakazi 18,627

**Na Claudia Kayombo, Iramba**

ZAIDI ya wakazi 18,600 wa Kata ya Kidaru Tarafa ya Kisiriri Wilaya ya Iramba mkoani Singida, wataondokana na adha ya kutembea umbali mrefu kufuata huduma za afya kufuatia kukamilika kwa ujenzi wa Kituo cha Afya cha Tygelo.

Kaimu Mganga Mkuu wa Wilaya ya Iramba, Dk. Timothy Sumbe, alisema ujenzi wa kituo hicho cha afya, umegharimu Sh. milioni 500 na kwamba wakazi 18627 wa kata hiyo, watanufaika na huduma hiyo.

Dk. Sumbe aliyasema hayo alipokuwa akizungumzia wakati wa uzinduzi rasmi wa kituo hicho mbele ya mgeni rasmi, Mkuu wa Wilaya ya Iramba, Yusufu Mwenda.

Alisema kuanza kutolewa huduma katika kituo hicho, kutawaondolea adha wananchi hao ya kufuata huduma za afya umbali mrefu walizokuwa wakikumbana nazo tangu kabla na baada ya Uhuru.

Katika hotuba yake, Mwenda alisema wananchi wa Iramba wan jukumu la kumheshimu Rais Dk. Samia Suluhu Hassan kwa kuwa amewaondolea adha hiyo kwa kuwezesha ujenzi wa Kituo hicho cha Afya.

Naye Diwani wa Kata ya Kidaru, Philip Manguli, alisema hatua ya kukamilika kwa ujenzi wa kituo hicho cha afya, inawaondolea wananchi shida ya huduma za afya waliyokuwa wanakumbana nayo kwa muda mrefu.

**kuanza kutolewa huduma katika kituo hicho, kutawaondolea adha wananchi hao ya kufuata huduma za afya umbali mrefu walizokuwa wakikumbana nazo tangu kabla na baada ya Uhuru.**




# Mmarekani kortini kwa kuishi nchini kinyemela

**Na Shamila Mkomweke, TURDACo**

RAIA wa Marekani, Yaki Juma, amefikishwa mahakamani akikabiliwa na mashitaka matano likiwemo la kutoa taarifa za uongo na kujipatia Kitambulisho cha Taifa.

Juma, alifikishwa katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu jijini Dar es Salaam juzi na kusomewa mashitaka yake mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu, Evodia Kyaruzi.

Wakili wa Serikali kutoka Idara ya Uhamiaji, Godfrey Ngwijo, alidai mahakamani hapo kuwa Septemba 14, mwaka huu, katika Ofisi za Uhamiaji Wilaya ya Ilala jijini Dar es Salaam, mshtakiwa huyo alibainika kuishi nchini bila kibali.

Ilidaiwa kuwa, katika tarehe na eneo hilo, mshtakiwa huyo akiwa akiwa raia wa Marekani, alitoa taarifa za uongo kwa maofisa wa Uhamiaji kuhusu utaifa wake kwa lengo la kujipatia hati ya kusafiria ya Tanzania.

Alielendelea kudai kuwa, katika tarehe hiyo na eneo hilo, Juma aliwasilisha nyaraka za kughushi kwa lengo la kujipatia cheti cha kuzaliwa na Kadi ya Taifa la Tanzania.

Katika shitaka lingine, ilidaiwa kuwa mshtakiwa huyo alitoa taarifa za uongo kuhusu uraia wake na kufanikiwa kupata Kadi ya Taifa la Tanzania.

Baada ya kusomewa mashitaka yake, mshtakiwa alikiri shitaka la kuishi nchini bila kibali, lakini alikana mashitaka mengine.

Mshtakiwa huyo alipelekwa mahabusu baada ya kushindwa kutimiza masharti ya dhamana likiwemo la kuwasilisha mahakamani hati yake ya kusafiria pamoja na wadhamini wawili wenye vitambulisho.

Kesi hiyo iliahirishwa hadi Septemba 22, mwaka huu kwa ajili ya kusomwa hoja za awali na maelezo ya shitaka alilokiri.

# Upelelezi wakwamisha kesi dawa za kulevya

**Na Shamila Mkomweke, TURDACo**

KESI ya Goodness Remmy na wenzake wawili wanaotuhumiwa kukutwa na kilo 58.68 za dawa za kulevya aina heroin, imeahirishwa Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu jijini Dar es Salaam, ikielezwa kuwa upelelezi wa shauri hilo, haujakamilika.

Hakimu Mkazi Mkuu, Amir Msumi, wa mahakamani hiyo, aliahirisha kesi hiyo baada ya Wakili wa Serikali, Asiath Mzamiru, kuomba tarehe nyingine ya kutajwa kwa kuwa upelelezi wake haujakamilika.

Pia alisema Mkurugenzi wa Mashitaka (DPP) amekwisha kupitia jalada la kesi hiyo, hivyo lipo katika mchakato wa kurejeshwa ili kuendelea na hatua nyingine.

Hakimu Mkazi Mkuu Msumi, pia alimtaka Wakili Mzamiru kueleza upelelezi umefikia hatua gani ili watuhumiwa wajue kesi yao imefikia wapi.

Washtakiwa wengine katika kesi hiyo ni Emmanuel Chigbo na Paulina Mwanga wanaodaiwa kutenda kosa hilo Aprili 19, mwaka huu, eneo la Salasala wilayani Kinondoni.

Inadaiwa kuwa, wakiwa eneo hilo, washtakiwa walikutwa wakisafirisha kilo 58.68 za heroin.

Kesi hiyo iliahirishwa hadi Oktoba 3, mwaka huu, itakapotajwa tena.

# ‘Kasi utengenezaji mabehewa treni mwendokasi inaridhisha’



**Na Mwandishi Wetu**

NAIBU Katibu Mkuu Wizara ya Wizara ya Fedha, Amina Khamis Shaaban, ameeleza kuridhishwa na maendeleo ya utengenezaji wa mabehewa na vichwa vya treni na treni ya mwendokasi.

Mabehewa na vichwa hivyo vya treni ya mwendokasi, vinatengenezwa na kampuni za Hyundai Rotem na Sing Sung Rolling Stock Technology (SSRST) za Korea Kusini.

Aliyasema hayo baada ya kutembelea kampuni hizo zilizopo katika mji wa Changwon, Korea ya Kusini, zilizoingia mkataba na Serikali ya Tanzania wa kutengeneza mabehewa 59 na vichwa vya treni 17 pamoja treni 10 za mwendokasi.

‘‘Kwa kampuni zote mbili, maendeleo ni mazuri kwa hatua iliyofikiwa na wametueleza kuwa wanatarajia kukamilisha utengenezaji wa mabehewa na vichwa vya treni kama ilivyoainishwa katika makubaliano. Na kwa kweli tuliyoyaona yako katika hali nzuri,” alisema Amina.

Aidha, aliielekeza sekta husika kuhakikisha kuwa inatoa mafunzo kwa watakaohusika na kuendesha, kuhudumia treni hizo, wanajengewa uwezo ili ziweze kudumu kwa muda mrefu na kutoa huduma bora kwa uendelevu.

‘‘Tunashauri wenzetu watakaosimamia uendeshaji wa treni hizi kwa Tanzania, wajengewe uwezo wa uendeshaji na utunzaji ili mabehewa na vichwa viendelee kuwa na ubora huu kwa ajili ya huduma na pia yaweze kudumu kwa muda mrefu,” alisisitiza.

Ujumbe wa Tanzania ulikuwa Busan Korea ya Kusini kuhudhuria mkutano wa saba wa Ushirikiano wa Kiuchumi kati ya Korea Kusini na Nchi za Afrika (KOAFEC), Mjini Busan, Jamhuri ya Korea Kusini ambapo Tanzania iliungana na nchi nyingine za Afrika katika mkutano huo.

# Singida yaweka mkakati izalishe mazao mseto

**Na Claudia Kayombo, Singida**

MKUU wa Mkoa wa Singida, Peter Serukamba, amesema mkoa wake unatekeleza mkakati wa kuuingiza katika

ramani ya mikoa inayozalisha kwa wingi mazao mbalimbali ya chakula na biashara kama ilivyo Mikoa ya Kusini.

Serukamba aliyasema hayo hivi karibuni mkoani hapa na kufafanua kuwa hilo linatokana na mkoa huu kuzalisha aina mbalimbali za mazao ya chakula na biashara, lakini si miongoni mwa mikoa inayozalisha kwa wingi mazao hapa nchini.

“Nataka mwaka huu Singida iingie katika ramani ya wazalishaji wa mazao mbalimbali kama ilivyo kwa Mikoa ya Kusini. Nataka Singida izalishe kwa wingi zaidi mazao kama alizeti, mahindi, dengu, mpunga na ufuta ambayo yatalisha Singida na nchi nzima kwa ujumla,” alisema.

Alibainisha kuwa hilo litawezekana kutokana na sababu mbalimbali ikiwa ni pamoja na ujenzi wa barabara mbalimbali katika kiwango cha lami zitakazochochea kufungua fursa mbalimbali za kilimo nchini.

# Watoto 608 watibiwa utapiamlo na kupona

**Tumekuwa tukifanya kazi na mradi wa USAID Afya Yangu RMNCAH ili kuhakikisha tunaboresha afya ya watoto ambapo tumewajengea uwezo watumishi wetu na wahudumu wa afya ngazi ya jamii ambao wanatusaidia kuwatambua watoto wenye utapiamlo na kuwaunganisha na tiba.**

**Na Mwandishi Wetu, Musoma**

WATOTO 608 kati ya 1,090 waliokuwa wakitibiwa ugonjwa wa utapiamlo mkoani Mara katika kipindi cha mwaka 2022, wamepona.

Mganga Mkuu wa Mkoa Mara, Dk. Zabrone Masatu, aliyasema hayo wakati akitoa ripoti za jitihada zinazofanywa na serikali kwa kushirikiana na wadau katika kutoa elimu kwa jamii na kuboresha huduma za afya kwenye vituo vya afya na hospitali mkoani humu.

Dk. Masatu alisema serikali kupitia mradi wa USAID Afya Yangu (RMNCAH), ilifanikiwa kutoa matibabu ya utapiamlo unaotokana na lishe duni hususani kwa watoto.

Alisema baadhi ya watoto wenye utapiamlo, wamekuwa wakichelewa kupata matibabu kutokana na imani za kishirikina na hivyo kuwapeleka kwa waganga wa tiba asili wakidhani wamerogwa, hali ambayo huchelewa kupata tiba sahihi ya chakula lishe.

Dk. Masatu alisema kutokana na imani hiyo, zaidi ya watoto 20 waliobainika kuwa na ugonjwa wa utapiamlo, wamekatisha matibabu ambapo jitihada za kuwafuatilia zinaendelea kupitia kwa watoa huduma za afya ngazi ya jamii ambao wamepewa mafunzo na wamekuwa wakiwabaini pia watoto wenye utapiamlo.

“Tumekuwa tukifanya kazi na mradi wa USAID Afya Yangu RMNCAH ili kuhakikisha tunaboresha afya ya watoto ambapo tumewajengea uwezo watumishi wetu na wahudumu wa afya ngazi ya jamii ambao wanatusaidia kuwatambua watoto wenye utapiamlo na kuwaunganisha na tiba,” alisema Dk. Masatu na kuongeza:

“Pia kupitia mradi wa USAID Afya Yangu- RMNCAH tumepata vibao 52 kwa ajili ya kutusaidia kupima viashiria vya utapiamlo kwa watoto katika vituo vyetu vya afya, tuinashukuru serikali kupitia mradi huu kila halmashauri katika mkoa wetu sasa ina Afisa Lishe anayesaidia kwenye utoaji huduma na kuwaelimisha wananchi kuandaa chakula lishe

Naye Afisa Lishe wa Halmashauri ya Bunda Mji katika Wilaya ya Bunda mkoani Mara, Lucy Mwaluwyo, alisema wakati mradi wa USAID Afya Yangu RMNCAH unaanza, kwa mwezi zaidi ya watoto 16 walikuwa wakitibiwa katika Hospitali ya Bunda DDH na Manyamanyama tofauti na sasa ambapo idadi hiyo imepungua kwa wastani wa watoto sita hadi wanane kwa mwezi.

Mwaluwyo alisema tayari alifanya kikao na waganga wa kienyeji na kuwaelimisha ili wanapoona mtoto mwenye dalili za utapiamlo ambazo ni pamoja na kunyong’onyea na mwili kuishiwa nguvu, wawashauri wazazi kuwapeleka hospitalini.

Mmoja wa wakazi wa Kijiji cha Guta wilayani Bunda, Regina Samson, alisema baada ya mwanawe kuugua utapiamlo, hakujua ni ugonjwa gani, hivyo ndugu walimshauri ampeleke kwa mganga wa kienyeji ambapo hata hivyo, baada ya kumfikisha huko, hakupona na hali yake ilizidi kuwa mbaya.

Baada ya Regina kuona hali ya mwanawe inazidi kubadilika, alimpeleka katika Hospitali ya Bunda DDH ambapo alibainika kuwa na ugonjwa wa utapiamlo na kuanzishiwa tiba ya chakula lishe iliyomsaidia kupona kabisa baada ya wiki tatu.

“Wahudumu Hospitali ya Bunda DDH walitufundisha jinsi ya kutengeneza uji wa lishe kwa kutumia mtama, mchele, mbegu za maboga, michembe, karanga, soya na ufuta. Sasa anaendelea vizuri, nawashauri wananchi wenzangu kwamba si kila kitu ni kukimbilia kwenye mitishamba ama kwa waganga wa kienyeji,” alisema Regina.

Mganga Mkuu mkoani Mara, Dk. Masatu alibainisha kuwa kabla ya mradi wa USAID Afya Yangu RMNCAH kuanza, matibabu ya utapiamlo yalipatikana katika Hospitali ya Rufaa Mkoa wa Mara, iliyopo wilayani Musoma na ile ya Shirati iliyopo wilayani Rorya, lakini baada ya mradi huo, matibabu yanapatikana katika vituo vinne vya afya na hospitali 11, hatua ambayo imeondoa hatari kwa watoto chini ya miaka mitano kupoteza maisha kutokana na ugonjwa huo.

Dk. Masatu alisema kupitia mradi huo wa USAID Afya Yangu RMNCAH, pia wanajamii walifundishwa namna ya kuandaa vyakula vyenye lishe ambavyo vinapatikana katika mazingira yanayowazunguka ikiwemo dagaa, mtama, karanga, mhogo na mahindi, hatua iliyosaidia idadi ya watoto wanaougua utapiamlo kupungua.

Jarida hili haliuzwi

*Leo yetu ndiyo kesho yetu*

Uelekeo

JARIDA

# Jungu Kuu

| Jumatano Septemba 20 - 26, 2023 |




# Ilichovuna Tanzania Mkutano wa AGRF 2023

UK. 12 & 13



UK. 14

UK. 15

Elimu

# Afichua siri kufuta ufaulu wa D na E



**Aidha, tuliondoa dharura zisizo na msingi za walimu, mwalimu akitoka shuleni labda ana msiba au mgonjwa ama anauguliwa na mtu wake wa karibu.**

**Na Claudia Kayombo, Singida**

BAADA ya kufundisha shule za serikali kwa zaidi ya miaka 36, sasa anatarajia kustaafu huku akiacha alama katika shule alizowahi kufanya kazi

kutokana na utendaji kazi wake mzuri kwa mujibu wa baadhi aliyowahi kufanya nao kazi katika taaluma hiyo.

Huyu si mwingine, bali ni Mwalimu Yessaya Ramadhani, anayetarajia hivi karibuni, kustaafu kwa mujibu wa sheria akiwa Mwalimu Mkuu wa Shule ya Msingi Ukombozi, iliyoko Manispaa ya Singida.

Mmoja wa walimu aliyowahi kufanya nao kazi, Lissu Mnyambi, anasema alifanya kazi na Mwalimu Ramadhani kwa miaka tisa katika Shule ya Msingi Nyerere.

Mwalimu Mnyambi anasema mara nyingi shule yao ilikuwa inaongoza kiwilaya na kimkoa.

"Tangu mwaka 2007 hadi 2016, mwenzangu alikuwa Mwalimu Mkuu nami nikiwa Mwalimu wa Taaluma na kwa hakika, shule yetu haikuwahi kushika nafasi zaidi ya 10 bora kiwilaya na wakati mwingine hata kimkoa.

"Kuna wakati serikali ilikuwa na utaratibu wa 'Lipa

Kulingana na Matokeo' ambapo shule zilizokuwa zinafanya vizuri, zilipewa fedha, Shule yetu ya Msingi Nyerere, tulipewa Sh. milioni 192 ambazo tulizitumia kujengea madarasa manne na matundu 20 ya vyoo kati ya hayo, 13 ya wasichana na saba ya wavulana.

"Mkakati wa Futa D na E tulioanzisha kwa usimamizi wa Mwalimu Mkuu, Ramadhani, uliwafanya walimu kupambana sana katika suala la ufundishaji.

"Pia Mwalimu wetu Mkuu, aliweka utaratibu wa kukutana na walimu wa masomo yote mara kwa mara kupeana mbinu za ufundishaji. Kwa jumla, kulikuwa na ushirikiano thabiti baina yake na walimu wengine.

"Kadhalika, kulikuwa na mitihani ya mara kwa mara ya ujirani mwema ambapo wakati fulani, zaidi ya shule 20 zilikuja kufanya mitihani na Shule ya Nyerere, tisa zilitoka Arusha baada ya shule yetu kujulikana huko kutokana na ufaulu mzuri," anasema Mwalimu Mnyambi.

Anabainisha kuwa Vilevile, michezo na utaratibu wa kula chakula shuleni ulioanzishwa shuleni hapo mapema, ulisaidia kupunguza utoro kwa kiasi kikubwa hata ambao hawakuwa wanapenda masomo, walikuja shuleni.

"Kulikuwa na ziara za kimafunzo katika maeneo mbalimbali ikiwamo katika mbuga za hifadhi. Tuliwahi kwenda Ngorongoro, Manyara, Tarangire na Ruaha.

"Pia ili kufanikisha ziara hizo na mikakati mbalimbali ya kimasomo tuliyokuwa tunaianzisha, ilikuwa inafanikiwa kwa sababu wazazi kwa wanafunzi walio wengi, waliunga mkono jitihada mbalimbali za kimasomo zilizoanzishwa na walimu kuchochea ufaulu mzuri," anasema na kuongeza:

"Na hii ndiyo siri ya kufanya vizuri mwaka hadi mwaka."

Anaongeza kuwa kutokana na shule hiyo kufundisha vizuri na hivyo kuwa na ufaulu wa juu mara nyingi, ongozeko la wanafunzi nalo lilikuwa kubwa.

Mwalimu Mnyambi anasema sifa ya ufaulu mzuri, uliotokana na mbinu za ufundishaji pia wakati fulani uliwawezesha wanafunzi wa darasa la saba katika Shule ya Msingi Mughumbu iliyoko Halmashauri ya Ikungi kwenda kuchanganyika na wanafunzi wa shule hiyo ambapo walikuwa wanafundishwa pamoja kwa mwezi mzima.

Anasema baada ya Mwalimu Ramadhani kuhama katika shule hiyo, baadhi ya shule zilizokuwa na utaratibu wa kufanya mitihani ya daima ya ujirani mwema, ziliacha na kwamba zinashuhudia kuwa hata ufaulu wao umeshuka pia.

Magdalena Kiula, aliyekuwa Mwalimu wa Taaluma katika Shule ya Msingi Ukombozi, anasema amefanya kazi kwenye nafasi hiyo katika kipindi cha miaka saba tangu 2016 hadi Machi, mwaka huu na Mwalimu Ramadhan akiwa Mkuu wake wa kazi.

Anasema Shule ya Msingi Ukombozi, imekuwa ikifanya vizuri katika kipindi hicho kutokana na Mwalimu Mkuu Ramadhan kujenga umoja miongoni mwa walimu na hivyo kushirikiana vizuri katika kufundisha wanafunzi wao.

"Pia majaribio ya kila wiki na mwezi ambapo walimu hufanya masahihisho ubaoni, yamechangia kuongeza uelewa wa watoto na hivyo kufanya vizuri katika mitihani yao.

"Aidha, tuliondoa dharura zisizo na msingi za walimu, mwalimu akitoka shuleni labda ana msiba au mgonjwa ama anauguliwa na mtu wake wa karibu. Na tulihakikisha kila mwanafunzi ana kitendea kazi, kwa wachache waliokuwa wanaishi na babu na bibi kutokana na kufiwa na wazazi wao, walimu walikuwa wanawanunulia kuanzia unifomu zao," anasema.

"Walimu tulikuwa tunakutana kujadiliana mambo mbalimbali ikiwamo mada ngumu katika masomo tunayofundisha na ikiwa mada fulani katika somo la

mmoja wa walimu haijui vizuri, mwalimu anayoiwezaalikuwa anakwenda kuifundisha kwa ufasaha. Pia walimu walikuwa makini kuzingatia muda wa vipindi," anasema Magdalena.

Kadhalika, anasema katika kuonesha mfano kwa vitendo, Mwalimu Mkuu Ramadhani alikuwa mhamasishaji mkuu katika utendaji kazi wenye mafanikio, alikuwa anaonesha mfano wa kushiriki vipindi mbalimbali darasani.

"Mwalimu Mkuu mwenyewe hakuwa anatega hata kidogo, hata walimu walio dhaifu katika utendaji kazi wao walishindwa kutega," anasema.

Anaeleza kuwa pia yeye akiwa mwalimu waTaaluma, alikuwa anafuata nyayo za Mwalimu Mkuu wake Ramadhan, alikuwa anafundisha somo la sayansi kwa ufasaha mkubwa na hivyo miongoni mwa aliowafundisha wapo ambao ni marubani wa ndege hivi sasa.

Khairath Muro, mwanafunzi wa darasa la saba katika shule hiyo, anasema darasa lao halina watoro kwa sababu waliokuwa na tabia hiyo, walichapwa viboko na sasa wamenyooka, wanahudhuria darasani vizuri.

"Walimu wetu wanatufundisha vizuri sana, hakuna wanafunzi watoro, tukifeli tunachapwa, tukiwa watoro wanatuchapa. Sasa watoro hawapo, wanaogopa fimbo kutoka kwa walimu," anafafanua mwanafunzi huyo.

"Binafsi, nawashukuru sana walimu wangu wote, wamenifundisha vizuri elimu ya darasani, nidhamu na wamenilea katika maadili mazuri," anasema Khairath.

Mwalimu Ramadhan alitarajia kuanza likizo ya kustaafu mwezi uliopita.

Hata hivyo, anasema akistaafu, ataimiss' kazi yake ya Ufundishaji.

Anasema iwapo angewapata wafadhili, angejenga shule ambayo angeisimamia vema, lengo likiwa ni kupata wanafunzi bora.

**CHANGAMOTO ALIZOKUTANA NAZO KAZINI:**

Anasema alikutana na nyingi baadhi zilitaka kumkatisha tamaa, lakini hakurudi nyuma badala yake alisonga mbele.

Katika kipindi hicho chote cha miaka 36, Mwalimu Ramadhan hajawahi kufanya kazi nje ya Mkoa wa Singida.

Mbali ya kufundisha Shule za Msingi Ukombozi na Nyerere, shule nyingine alizofundisha ni Unyakindi, Singidani, Unyianga, Unyambwa, Kititimo, Ipungi, Uhamaka na Ughaugha.

Moja ya changamoto kubwa ambayo anasema hataisahau wakati yupo katika Shule ya Msingi Unyambwa ambapo alipohamishiwa kama mwalimu, aliambiwa kuwa shule hiyo haifaulishi.

"Niliambiwa na wazazi kuwa shule hiyo watoto wao hawafaulu, wakifaulu, majina yao yanabadilishwa na kupewa watoto wengine wa shule nyingine, hivyo nisijisumbue kuhusu ufaulu wa watoto," anasema na kuongeza:

"Nikaweka mkakati wa kuhakikisha nafundisha hadi wanafunzi wanafaulu na ndipo mwaka huo ilikuwa 1994, walipofaulu saba, mwaka uliofuata walifaulu 12, lakini pamoja na jitihada hizo nzuri, nilikuwa napigwa vita."

Elimu

# Kibaha waita wadau uboreshaji wa elimu

**Na Mwandishi Wetu**

BABA wa Taifa, Mwalimu Julius Nyerere ambaye siku chache zijazo tutaadhimisha miaka 24 ya kifo chake, alipata kusema kwamba ukitaka kumsaidia mtoto wa maskini, mpe elimu.

Ni katika muktadha huo, Seikali imeendelea kumwezi Mwalimu kwa kuja na mikakati kabambe ya kuboresha miundombinu ya elimu sambamba na ujenzi wa shule za sekondari ngazi ya kata ili wanafunzi wanaofaulu waweze kupata nafasi ya kusoma.

Afisa Elimu Mkoa wa Pwani, Sara Mlaki anapongeza mikakati ya Rais Samia katika sekta ya elimu ambayo inawezesha sasa wanafunzi kuanza kidato cha kwanza takribani wote. Hii huko nyuma ilikuwa hajawahi kutokea na ndio maana kukawa na msemo wa 'wanaochaguliwa' na siyo 'wanaofaulu'.

Hii maana yake ni kwamba tumepitia vipindi ambavyo vijana wakiwemo watoto wa maskini walikuwa wanafaulu kwa viwango vilivyowekwa lakini wanakosa nafasi ya kuendelea na masomo ya sekondari kwani 'wanaochaguliwa' ni wachache kutokana na uchache wa madarasa!

Sara anasema hatua ya sasa ya serikali ya Rais Samia Suluhu Hassan inatoa nafasi kwa wanafunzi wa shule za msingi kusoma kwa bidii ili waweze kujiunga na kidato cha kwanza wakiwa hawana hofu ya kukosa nafasi.

Sara anasema kwa sasa kazi iliyopo ni kupambania ujenzi wa mabweni kwenye shule ambazo zipo mbali na makazi ili wanafunzi wapate muda wa kujisomea na kupunguza tatizo la utoro.

Katika Mkoa wa Pwani wapo wanafunzi wamekuwa wakikatisha masomo kwa sababu mbalimbali ikiwemo ya kushindwa kumudu kutembea umbali mrefu ama vishawishi wanayokutana navyo wanapokuwa njiani wakitoka ama kwenda shule. Umbali mrefu wa kutoka nyumbani hadi shule umekuwa pia ukitajwa kama sababu ya wanafunzi, hususani wasichana kurubuniwa na vijana wa hovyo na kujikuta wakipata mimba za utotoni na kuharibu kabisa ndoto zao.

Jitihada za kuwanusuru wanafunzi na kero hiyo zimekuwa zikifanyika katika maeneo mbalimbali ikiwemo Kibaha katika Kata ya Mbwawa.

Diwani wa kata hiyo, Judith Muluge anasema amelazimika kuvalia njuga suala la ujenzi wa mabweni ikiwa ni pamoja na kuwasaka wafadhili ili kunusuru wanafunzi, hususani wasichana na 'zimwi' la umbali mrefu.

Muluge anaeleza kwamba Shule ya Sekondari ya Mbwawa Miswe wapo wanafunzi ambao wanakabiliwa na adha hiyo ya umbali mrefu na kwamba wengi wanachelewa kufika darasani kwa wakati.

Kutokana na hali hiyo diwani huyo amekuwa akitafuta wafadhili ambao watashirikiana na wananchi kujenga mabweni ili wanafunzi wawe karibu na mazingira ya shule na hivyo kuwawezesha wanafunzi wote kuanza masomo kwa wakati mmoja.

Katika mapambano yake, diwani amefanikiwa kuanzisha ujenzi wa bweni la wasichana kwenye shule hiyo hadi kufikia ngazi ya msingi.

Moja ya wafadhili waliopatikana ni taasisi ya Rehema Foundation ambao wametembelea shule hiyo na kujiridhisha na jitihada zilizofanywa na wananchi.

Rehema Foundation mbali ya kukubali kushirikiana na wananchi na diwani huyo kukamilisha ujenzi wa bweni hilo pia wameahidi kutatua kero ya maji kwa shule zenye kikwazo hicho.

"Nimeamua kushirikiana na wananchi kwa kuwa mimi ni mwakilishi wao. Mbali ya kunituma kufikisha kero zao halmashauri pia wameniomba kutafuta wafadhili wa kusaidia kutatua vikwazo kwenye kata yetu," anasema Muluge.

Muluge anaeleza kwamba baada ya kuzungumza na taasisi hiyo alielekezwa kuwashirikisha madiwani wengine wenye vikwazo kama hivyo ili vitafutiwe ufumbuzi.

Mwakilishi wa Rehema Foundation, Zuberi Salum anasema kwamba baada ya kupokea mahitaji ya madiwani kwenye shule zilizopo katika kata zao wanajipanga kutafuta mashirika mengine watakayoshirikiana nayo kutafuta ufumbuzi wa kero hizo.

Salum pia anawasihi wananchi kuchangia katika shughuli za maendeleo ikiwemo sekta ya elimu badala ya kuacha jukumu hilo kufanywa na serikali pekee kwani nayo ina majukumu chungu mzima.

Mkuu wa shule ya Mbwawa Miswe, Getrude Hamaro anasema kwamba shule hiyo ina uhitaji mkubwa wa mabweni ili kuwawezesha wanafunzi kupata muda wa kujisomea lakini pia kuwahi vipindi vya masomo.

Hamaro anasema wapo wanafunzi wanafika saa mbili hadi saa tatu shuleni kutokana na kuishi mbali na wengine kushindwa kuvuka mto Ruvu kwa wakati kwa kukosa kivuko cha uhakika.

"Uwepo wa mabweni shuleni kwetu utasaidia pia kuwaepusha wanafunzi katika hatari ya vishawishi vinavyosababisha wapate mimba kutokana na kutembea umbali mrefu kuja shule na kurudi nyumbani," anasisitiza.

Mmoja wa wanafunzi wa shule hiyo, Rehema Yassin anaomba wadau wa elimu kujitokeza kuwasaidia kujenga bweni kwani kwa sasa wapo wanaoishi ng'ambo ya mto Ruvu ambapo asubuhi wanachelewa vipindi wanapokuta mtumbwi tayari uko upande wa pili.

Aidha anasema wanafunzi wanaoishi mbali na shule wanachelewa kurudi nyumbani na kwamba kutokana na majukumu mengine wanakosa muda wa kujisomea.

Mwanafunzi mwingine wa shule hiyo, Ezekiel Bashiri, anabainisha kwamba wakati wa asubuhi wanafunzi wanachelewa kutokana na vyombo vya usafiri kukataa kuwabeba kwa sababu ya nauli ndogo wanayolipa.

Anasema uwepo wa mabweni utawasaidia kupata muda wa kujisomea na kuongeza ufaulu kwenye shule yao sambamba na kuondokana na vikwazo wanavyokumbana navyo kwa sasa njiani.

Hamis Mohamed, mmoja wa wazazi wanaoishi Kata ya Miswe anasema pamoja na wazazi kuwa tayari kushiriki kuchangia, ni muhimu wadau wa elimu wajitokeze kusaidia katika kuwanusuru wanafunzi na adha hiyo.

Katika shule ya Mbwawa Miswe, mbali ya ukosefu wa mabweni unaosababisha baadhi ya wanafunzi kutembea umbali wa kilomita sita mpaka nane, pia kipo kikwazo cha upatikanaji wa maji ya uhakika.

Maji yamekuwa pia yakitajwa kuwa kikwazo kikubwa kwa wanafunzi wa kike hasa wanapokuwa katika hedhi, hali inayowafanya wahitaji sana maji kwa ajili ya usafi.



**Uwepo wa mabweni shuleni kwetu utasaidia pia kuwaepusha wanafunzi katika hatari ya vishawishi vinavyosababisha wapate mimba kutokana na kutembea umbali mrefu kuja shule na kurudi nyumbani.**

## Uchumi



# Ilichovuna Tanzania Mkutano wa AGRF 2023

**Na Boniface Luhanga**

MKUTANO wa Jukwaa la Mifumo ya Chakula Barani Afrika (AGRF) kwa mwaka huu, ulifanyika katika Kituo cha Mikutano cha Kimataifa cha Julius Nyerere (JNICC) jijini Dar es Salaam kuanzia Septemba 5 na kuhitimishwa Septemba 8, mwaka huu. Mkutano huo ulilenga kujadili mabadiliko ya mifumo ya chakula na kuhakikisha kunakuwepo na uhakika wa chakula kwa wote.

Septemba 6, mwaka jana, mkutano kama huu ulifanyika jijini Kigali, Rwanda.

Kimsingi, AGRF ni Jukwaa Kuu la Kilimo Afrika linalowaleka pamoja wadau wa sekta ya kilimo na kujadili pamoja na kubadilishana mawazo mambo yatakayosaidia kilimo katika Bara la Afrika ili kizidi kukua.

Mkutano wa jijini Dar es Salaam, uliwakutanisha zaidi ya washiriki 3,000 kutoka nchi zaidi ya mataifa 70 Afrika na watoa mada zaidi 350 wakiwemo viongozi wakuu wa nchi, mawaziri wa kilimo, wataalam na wanasayansi mbalimbali kutoka nchi hizo.

Ushiriki mkubwa wa viongozi wakuu wa nchi, mawaziri wa kilimo na wanasayansi waliobobea katika masuala ya kilimo, ulitoa fursa kubwa kwa Tanzania kujifunza mengi yahusuyo masuala ya mifumo na usalama wa chakula nchini.

Tanzania inaamini kwamba kilimo ni uti wa mgongo wa uchumi kwani pia sekta hiyo inachangia zaidi ya asilimia 60 katika ajira kwa vijana na wanawake,

Tayari Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, imebuni mpango wa jenga kesho iliyo bora (Build a Better Tomorrow - BBT), na mpaka sasa wapo vijana zaidi ya 800 wakiendelea na mafunzo na shughuli za kilimo kupitia mpango huo.

Akihutubia katika mkutano huo Septemba 7, mwaka huu kwa ngazi ya marais, Rais Dk. Samia alizihimiza nchi za Afrika kushirikiana ili kukabiliana na aibu ya baa la njaa kutokana na bara hilo kuwa na asilimia 65 ya ardhi inayofaa kwa kilimo duniani.

Rais pia alisema Afrika ina asilimia 60 ya utajiri wa rasilimali na maziwa makubwa, nguvu kazi ya kutosha ya vijana na madini yanayoweza kuingizia fedha nyingi za kuwekeza katika kilimo.

Rais Samia anasikitishwa na hali ya Afrika ya kuwa bara la walalamikaji badala ya kuweka mikakati na kutafuta mbinu za kujiiletea mapinduzi ya kijani.

Anasema watu takribani milioni 283 barani Afrika, wanalala na njaa kila siku, wengine wanapata utapiamlo na baadhi yao kufariki dunia kwa kukosa chakula, jambo ambalo analitafsri kama ni la aibu na halikubaliki kwa dunia ya leo.

Kwa msingi huo, Rais Dk. Samia anazitaka nchi za Afrika kuzigeuza changamoto zinazoikabili dunia kuwa fursa kwao, kwa kuwekeza zaidi katika kilimo, hususani kwa kuwawezesha vijana na kuwatatulia matatizo yao.

Matatizo hayo yanayowakabili vijana ni pamoja na ukosefu





wa taarifa sahihi, ardhi, mitaji, athari za mabadiliko ya tabianchi na kuibuka kwa magonjwa duniani.

Anabainisha kuwa ili kufikia malengo ya usalama wa chakula barani Afrika, nchi za Afrika hazina budi kutathmini vipaumbele vyake na kutunga sera zinazoendena na mahitaji ya sasa ya dunia.

Anasema ni muhimu kwa nchi za Afrika kutekeleza ahadi ilizojiwekea ambazo zimebainishwa katika Progaramu ya Maendeleo ya Kilimo ya Umoja wa Afrika ya mwaka 2003, Azimio la Malabo la mwaka 2014 kuhusu kuongeza kasi ya ukuaji wa sekta ya kilimo na mikakati mingine kuhusu kilimo.

Miongozo ya maazimio hayo yanaelekeza nchi za Afrika kuongeza bajeti ya kilimo hadi asilimia 10, kukuza sekta ya kilimo kwa asilimia sita, kuimarisha ukuaji jumuishi wa sekta ya kilimo, kuhamasisha na kushirikisha sekta binafsi katika kilimo, kutoa fursa za ajira kwa vijana angalau kwa asilimia 30 katika minyororo ya uongezaji thamani katika mifumo ya kilimo na kuongeza biashara ya bidhaa na huduma za kilimo barani Afrika.

Rais Dk. Rais anaeleza kuwa Tanzania inatekeleza maazimio hayo kwa kuongeza bajeti ya sekta ya kilimo, kutekeleza ajenda 1030 ya kuongeza ukuaji wa sekta ya kilimo kwa asilimia 10 ifikapo mwaka 2030, kuingia katika masoko ya chakula ya kikanda na ya kimataifa ili kukidhi mahitaji ya chakula katika nchi mbalimbali.

Aidha, anaeleza kuwa ili kuchochea sekta ya kilimo nchini, serikali inatekeleza programu mbalimbali ikiwamo ya kuwawezesha vijana na wanawake kupitia mpango huo wa BBT iliyozinduliwa mwaka jana na inatekelezwa katika mikoa mbalimbali nchini.

Rais Dk. Samia ambaye aliungana na Rais wa Kenya, William Ruto, Rais wa Burundi, Evariste Ndayishimiye, Rais wa Senegal, Macky Sall na Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Mwinyi, aliahidi kuwa Afrika ipo tayari kuzalisha chakula cha kutosha na kuacha kutegemea bidhaa hiyo muhimu kutoka nje.

**MADA ZILIZOJADILIWA:**

**Sekta za Mifugo na Uvuvi:** Mada hii iliunganisha wadau wakubwa kwenye sekta. Ilijadili sekta kwa ujumla na kuainisha mwelekeo na vipaumbele. Wazungumzaji walikuwa ni kutoka Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Mpango wa Kuendeleza Kilimo Ukanda wa Kusini mwa Tanzania (SAGCOT) na Heifer International.

**Good Morning AGRF:** Mada hii iliuwa ni ya kila siku asubuhi wakati wa kuanza vikao. Ililenmga kuonesha kwa kifupi yaliyojiri siku iliyotangulia na yatakayojiri siku hiyo. Waandaaji walikuwa ni Jolenta Joseph wa Tanzania, John Agboola kutoka Nigeria na Wangari Kuria kutoka Kenya.

**Tengeneza upya, chukuua hatua:** Ufumbuzi wa mabadiliko ya mifumo ya chakula Afrika (Recover, Regenerate, Act: Africa's Solutions to Food Systems Transformation): Lengo la mada hii ilikuwa kuweka msingi wa AGRF 2023, kuunganisha wadau mbalimbali wenye malengo na uzoefu tofauti.

Katika kikao cha kujadili mada, uzinduzi wa Ripoti ya Kilimo Afrika (Africa Agricultural Report) ulifanyika. Mada ndogondogo zilijadiliwa pia ambapo wazungumzaji walikuwa ni Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dk. Philip Mpango na Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega.

Uzinduzi wa Jukwaa dogo la kujadili suala mahsusi la ufadhili wa kilimo:

Wadau wakuu kuhusu upatikanji wa fedha na jamii ya wafanyabiashara, walikutana na kubadilishana mawazo kuhusu uwekezaji katika kilimo.

Wazungumzaji walikuwa ni Naibu Waziri wa Fedha, Dk. Ashatu Kijaji IFC, Janngo Capital & led Financial Business Award Winner CEO Forum 2023, Pearl Capital Partners Ltd, MyGrowthFund Venture Partners, Benki Kuu Tanzania, mwakilishi kutoka Serikali ya Kenya, IFAD, Rwanda Development Board, AFEX na USAID.

Katika mkutano huu wa AGRF 2023, baadhi ya faida ambazo Tanzania ilifanikiwa kuzivuna ni:-

**(i) Kupatikana kwa masoko mapya ya mazao ya kilimo:** Tanzania itanufaika na kuchochea uzalishaji wa mazao ya kilimo kama vile alizeti, pamba, karafuu, viungo, matunda na mbogamboga kutokana na kuongezeka kwa soko la bidhaa ambazo zitazalishwa nchini.

**(ii) Kuimarika kwa mnyororo wa thamani wa mazao ya kilimo:** Kuna matarajio ya kuimarika kwa mnyororo wa thamani wa mazao ya kilimo ambayo mengi yanahusisha wakulima wadogo. Hii itasaidia kuongeza tija na ubora kwa bidhaa na huduma za Tanzania kutokana na kuongeza kwa ushindani na hivyo kuwezesha kupungua kwa bei za bidhaa.

**(iii) Uwekezaji katika mlolongo wa thamani ya mifumo ya chakula:** Tanzania inayosifika kwa uzalishaji wa chakula katika eneo la Afrika Mashariki, inalenga kuongeza ushirikiano na kukaribisha uwekezaji katika mlolongo wa thamani ya mifumo ya chakula. Hii itasaidia kuviendeleza viwanda, Viwanda vidogo na biashara ndogo na uhawilishaji wa teknolojia kutoka nje ya nchi (technology transfer) kutokana na uwekezaji utakaofanyika nchini.



# Hatuna sababu kuagiza matufaa nje

**Na Lauden Mwambona, Mbeya**

NI Jumamosi jioni, nikiwa katika matembezi ya kawaida, napita katika stendi ya daladala ya Mwanjelwa jijini Mbeya ambapo ninakuta vijana na akina mama wakiuza aina mbalimbali ya matunda.

Pamoja na uwapo wa matunda mengine kama ndizi, machungwa, maparachichi na mbogamboga, jicho langu linavutika zaidi kuanagalia rundo la matunda aina ya tufaa (apples) yanayouzwa hapo.

Sijayala siku nyingi na hivyo navutika kununua moja. "Apple moja Sh. 1,000... unajua haya matunda yanatoka Afrika Kusini," anasema mmoja wa wauzaji wa matunda hayo anayejitambulisha kwa jina la Juliana Mwilu.

Akifafanua zaidi kuhusu ukubwa wa bei, Juliana anasema yeye anayafuata matunda hayo Tunduma mkoani Songwe, mpakani mwa Tanzania na Zambia. Huko anasema anayanunua yakiwa kwenye maboksi kwa bei ya jumla.

Hata hivyo, Juliana anasita kutaja bei anazonunulia, lakini anasisitiza kwamba tunda moja yeye analiuza kwa Sh 1,000. Hii maana yake ni kwamba akiuza matunda 10 anatia kibindoni Sh 10,000!

Naangalia upande mwingine wa stendi hiyo, nawaona wanawake wengine zaidi ya watatu wanaouza matunda hayo na alhamdulillahi, wateja wanapata. Hata wingi huo wa matunda unamaanisha kwamba soko lake si haba!

Hali hii inanikumbusha siku nilipopita kwenye mitaa kadhaa ya Dar es Salaam, hususani kwenye maeneo ambayo kuna foleni za magari kama pale njia ya kwenda Goba, kwenda Africana na Chang'ombe. Pembeni utaona vijana wanauza matufaa kwa watumiaji wa magari.

Nikirudi hapa Mbeya, miaka ya nyuma matunda ya tufaa yalikuwa yanauzwa kwenye maduka makubwa (supermarkets) lakini hivi sasa yametapakaa kwenye stendi nyingi za mabasi kuanzia Tunduma na Vwawa, mkoani Songwe hadi Mwanjelwa, Kabwe, Nanenane na Uyole mkoani Mbeya.

Ma-apple kama wengi wanavyopenda kuyaita pia yanapatikana kwenye vituo vingi vya mabasi mkoani Njombe na Iringa kwa bei ya kati ya Sh 500 na Sh 1,000 kwa tunda moja.

Kitendo cha kuuza tunda moja kati ya Sh 500 na Sh 1,000 wakati ni dogo kuliko baadhi ya machungwa kinafikirisha kwa namna moja au nyingine.

## MATUFAA HAYASTAWI NCHINI?

Ninajua yapo matufaa yanayolimwa Tanga lakini ninaambiwa ni madogomadogo na hayana soko kubwa kama haya ya Afrika Kusini. Sasa swali linakuija. Kwa nini tunaagiza haya matunda kutoka Afrika Kusini. Hatuwezi kuyalima hapa Tanzania?

Swali hilo ninamtupia mtalaamu wa masuala ya kilimo kutoka Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Mbeya ambaye hataki jina lake liandikwe gazetini lakini anasema miti ya matufaa ipo katika mikoa wa Njombe na Iringa ingawa, kama ilivyo Tanga, matunda yake ni madogomadogo. Anasema kwa udogo huo, bei yake iko chini na hayafanyi vizuri katika soko.

Anasema matunda haya yanastawi zaidi maeneo yenye ubaridi na joto kidogo na kwamba ndiyo maana Afrika Kusini ni wakulima wakubwa wa matunda hayo kutokana na hali yao ya hewa kuruhusu.

Hata hivyo, anadokeza kwamba kwa sasa nchini ipo kampuni mpya anayoitaja kwa jina la Tamutamu Tanzania ambayo imeanza kuhamasisha wakazi wa mikoa ya Iringa, Njombe na Mbeya kulima kilimo cha matufaa ya kisasa kama yanayotoka Afrika Kusini.

Ofisa Ugani wa kampuni hiyo ya Tamutamu Tanzania, Gibson Sospeter akizungumza kwa njia ya simu anasema ni kweli kampuni yao ipo maeneo ya Ifunda mkoani Iringa ikihamasisha kilimo cha matufaa.

"Hapa sisi tumeanza kuyalima miaka minne iliyopita na sasa tuna shamba la karibu ekari 30 ambalo mwaka huu tunatarajia kuzalisha tani 25 za ma-apple," anasema.

Anasema kampuni yao sasa imechukua jukumu la kuhamasisha kilimo cha matufaa nchini ili Watanzania wapate fedha na kuinua uchumi wa taifa ikiwezekana iwe sababu ya kutolazimika tena kuagiza matunda hayo nje ya nchi.

Sospeter anasema soko la matufaa nchini ni kubwa na kwamba ndio maana bei ni kubwa pia na hasa kwa kuwa matunda hayo yanatoka mbali.

Anasema kampuni yao ya Tamutamu Tanzania imepata soko pia nchini Marekani la matufaa na kwamba wanatakiwa kupeleka matunda hayo yakiwa yamesindikwa kwa kufanywa juisi pamoja na matufaa yaliyokaushwa.

## WATANZANIA CHANGAMKENI

"Kampuni ya Tamutamu Tanzania inaendelea kuhamasisha kilimo cha matufaa katika mikoa ya Mbeya, Iringa, Sumbawanga, Njombe, Simiyu na Tanga maeneo ya Lushoto," anasema.

Anasema kampuni yao pia inajenga kiwanda cha kusindika matufaa hayo pamoja na jengo la kuhifadhi ubaridi katika eneo la Ifunda na kwamba kiwanda kitahudumia matunda ya aina hiyo kutoka kwa wakulima pande zote za Tanzania.

Naye mshirika wa kibiashara wa kampuni ya Tamutamu Tanzania, David Runge ambaye ni raia wa Ujerumani anasema miti ya matufaa ya asili ipo mikoa ya Njombe na Iringa, lakini sasa wanaendelea kuleta vikonyo kutoka Afrika kusini, Marekani na Japan ili kuboresha miche ya miti ya asili na ya kisasa. Runge anasema kwa sasa wakulima wamelipia jumla ya miche 25,000 ambayo kila mche unauzwa Sh 10,000.

Ofisa huyo anaishukuru Serikali ya awamu ya sita chini ya Rais Samia Suluhu Hassan kwa kusisitiza umuhimu wa kilimo na kwamba tayari Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe ameahidi kuweka mkono wake kwa kutilia mkazo kilimo cha matufaa nchini ili Watanzania wapate zao jipya litakalowaingizia fedha.

## MANUFAA YA KIAFYA

Kwa mujibu wa taarifa za mitandaoni matufaa yana faida nyingi kwenye mwili wa binadamu. Baadhi ya faida hizo zinatajwa kuwa ni kuupa mwili Vitamini K, nyuzi lishe pamoja na dawa lishe (phytochemicals) aina ya quercetin flavonoid.

Ni kwa msingi huo, taarifa hizo za mitandao zinaonesha kwamba matufaa yanasaidia wenye ugonjwa wa kuharisha, yanatibu uvimbejoto wa utumbo (colitis), yanazuia shinikizo la damu na pia husaidia kuzuia magonjwa ya mzio (allergy) na pumu ya mapafu.

Tufaa pia husaidia kuondoa choo kikavu au kutokupata choo (constipation), husaidia magonjwa ya moyo na mishipa ya damu, kuzuia mawe katika figo, kupunguza hatari ya kupata saratani ya mapafu, saratani ya utumbo na ugonjwa wa kisukari, kuuimarisha afya ya ini na pia matufaa husaidia figo kuondosha sumu aina ya uric acid ndani ya damu.





# Tanzania, Congo (DRC) zitakavyonufaika uondoaji viza

TAKRIBAN wiki mbili zilizopita, Serikali ya Tanzania ilitangaza kuondoa viza kwa raia wote wanaotoka Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC).

Uamuzi huo unawafanya raia wa nchi hizo kuwa na uhuru zaidi wa kuingia na kutoka kwa ajili ya biashara na mambo mengine.

Kwa mujibu wa takwimu za makadirio za Umoja wa Mataifa (UN) hadi kufikia mwaka huu, DR Congo inakadiriwa kuwa na watu milioni 102.

Ni taifa la nne Afrika kwa kuwa na idadi ya watu wengi nyuma ya Nigeria, Ethiopia na Misri. Na ni nchi ya 15 ulimwenguni kwa kuwa na watu wengi.


Licha ya Tanzania na DRC kupakana, raia wa nchi hizo wanaunganishwa na lugha ya Kiswahili.

Zaidi ya asilimia 90 ya Watanzania ni wazungumzaji wa Kiswahili na kwa upande wa DRC kuna wazungumzaji wa lugha hiyo wanaokadiriwa kufikia asilimia 40 ya raia wa nchi hiyo. Hawa wanapatikana zaidi katika mikoa ya mashariki mwa nchi hiyo.

DR Congo pia ni mwanachama wa karibuni wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC).

Kuondoa viza, kunaenda sambamba na malengo ya jumuiya hiyo ya kukuza biashara kati yao, vilevile kuwa na soko huru litakalorahisisha shughuli za mauzo na manunuzi.

Katika hesabu za kiuchumi, wingi wa watu ni jambo muhimu sana. Idadi kubwa ya watu katika nchi zote mbili, kunaweza kuifanya sekta ya biashara kukua maradufu, ikizingatiwa kuwa tayari nchi hizo zimekuwa zikifanya biashara baina yao kwa muda mrefu.



**USHIRIKIANO WA KIUCHUMI**

Kwa mujibu wa taarifa ya Hali ya Uchumi wa Taifa nchini Tanzania ya mwaka 2020, Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo, ndiyo inayoshika nafasi ya kwanza miongoni mwa nchi jirani kupitisha mizigo katika Bandari ya Dar es Salaam. Nchi hiyo hupitisha zaidi ya asilimia 30 ya mizigo yote.

Kutoka 2018 upitishaji huo umekuwa ukiongezeka mwaka hadi mwaka. Mwaka 2018, DR Congo ilipitisha tani milioni 1.8, mwaka 2019 tani milioni 1.9, mwaka 2020 tani milioni 1.8, mwaka 2021 tani milioni 2.4 na mwaka 2022 tani milioni 3.4.

Katika juhudi za kukuza biashara kati ya nchi hizi mbili, Waziri wa Fedha, Dk. Mwigulu Nchemba, alieleza Agosti, mwaka huu kuwa Tanzania inatafuta eneo kwa ajili ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo kupatiwa bandari kavu ya kuhifadhia mizigo ya nchi hiyo.

Kauli hiyo ilikuja baada ya mazungumzo na Waziri wa Uchukuzi na Mawasiliano wa DRC, Ekila Libombo, kuhusu mipango ya kuimarisha miundombinu ya usafiri na usafirishaji kati ya nchi hizo ili kukuza biashara na uchumi.

Mbali na Bandari ya Dar es Salaam, Mkoa wa Kigoma uliopo Kaskazini Magharibi mwa Tanzania karibu na fukwe ya mashariki ya Ziwa Tanganyika, pia ni lango kuu la kibiashara kati ya Tanzania na DRC.

Katika mkutano wa hadhara uliofanyika Mwanga Center mkoani Kigoma, Julai 2023, mwanachama wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) na Mbunge wa Ukonga, Jerry Silaa, ambaye hivi karibuni aliteuliwa kuwa Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, alisema:

"Kigoma ni lango la Tanzania. Ipo mizigo mingi sana inayopita kwenye Bandari ya Dar es Salaam kwenda DRC, Burundi na ili ifike vizuri, lazima ipite Kigoma."

**APONGEZA HATUA**

Mara baada ya Serikali ya Tanzania kutangaza kuondoa viza kwa raia wa DR Congo, mwanasiasa wa upinzani wa chama cha ACT Wazalendo na Mbunge wa zamani wa Kigoma Mjini, Zitto Kabwe, aliandika kupitia ukurasa wake wa kijamii wa Twitter maneno haya:

"Kwa miaka zaidi ya 10 nimekuwa nikipigania suala la wananchi wa Congo (DRC) kuingia nchini Tanzania bila malipo ya viza na vile vile Watanzania kwenda DRC bila malipo ya viza.

Hiki kilikuwa ni kilio kikubwa cha wafanyabiashara wa Kigoma ambao soko lao kubwa ni DRC. Nimefurahi sana kuwa hatimaye malipo ya viza yamefutwa. Biashara ya ukanda wa Ziwa Tanganyika itashamiri sana."

**FAIDA KWA MTU MMOJA MMOJA**

Mkoa wa Kigoma, ni lango kuu la kibiashara kati ya Tanzania na DRC. Biashara huendeshwa na watu, usafiri unapokuwa mwepesi wa kuingia na kutoka hata shughuli za kibiashara nazo zitazidi kuwa nyepesi.

Vilevile wapo ambao huingia kwenye nchi hizi kwa ajili ya masomo na matembezi. Pia, nao watanufaika kwa kuondolewa viza.

Uombaji wa viza hugubikwa na mchakato mrefu, hata baada ya kukamilisha mchakato huo, majibu yake wakati mwingine hayaji papo kwa papo. Humlazimu mtu kusubiri siku kadhaa au hata wiki kabla nchi husika haijakubali au kukataa maombi yake.

Nchi nyingi siku hizi zina utaratibu wa kuomba viza mtandaoni. Ila pia zipo zile ambazo mtu hulazimika aende ubalozi wa nchi husika.

Kuondolewa kwa viza maana yake msafiri hatohitajika tena kujaza fomu yenye mambo mengi ya kuomba viza na kusubiri majibu kwa siku kadhaa.

Fomu ambayo huambatanishwa na barua; mfano ya mwajiri wako, mwenyeji wako, picha ndogo au taarifa kutoka benki sasa haitakuwepo.

Mbali ya yote, viza inapoondolewa, hakutahitajika tena malipo ya kulipia viza kama ilivyo kwa nchi ambazo unatakiwa uilipie viza.

Tiketi ya ndege au basi na fedha za kujikimu, ndiyo mambo muhimu ya kuyazingatia.

Pia msafiri katika ya nchi atatakiwa kuwa na hati ya kusafiria na labda cheti cha kimataifa cha chanjo ambacho pia hujulikana kama 'kadi ya njano.'

Hii ni kusema kuwa kazi ya kusafiri kuingia na kutoka katika nchi hizi mbili itazidi kuwa nyepesi na shughuli za kibiashara zitakua.

***BBC.***

Siasa



# Mambo saba yanayochangia Watanzania kumwamini Samia

**Na Lauden Mwambona, Mbeya**

MCHAMBUZI wa masuala ya siasa, Baraka Mussa ameandika uchambuzi wake katika mitandao ya kijamii ya kundi moja sogozi la wasomi akiainisha mambo saba ambayo anaamini yanawafanya Watanznia kumpenda na kumwamini zaidi Rais Samia Suluhu Hassan.

Kwa kuwa wengi hawamo kwenye kundi sogozi hilo, makala haya yanaangalia tena mambo hayo kwa faida ya ambao hawakubahatika kuyasoma.

Mussa katika uchambuzi wake anaanza kwa kuangalia jarida la Forbes katika makala yake ya Machi 2022 ambayo ilimwelezea Rais Samia kama Rais wa Afrika wa aina yake na mfano wa kuigwa.

Forbes linasema Dk Samia ameonesha uongozi unaoendeleza demokrasia Tanzania na unaoleta maendeleo na matumaini makubwa kwa Tanzania.

Akiunga mkono mtazamo wa jarida hilo, Mussa anasema katika Bara la Afrika, Rais Samia ni kiongozi anayeleta athari chanya kwa maendeleo ya taifa na ustawi wa Watanzania.

Anasema Watanzania wana imani na matumaini makubwa katika uwezo wake wa kuliongoza taifa kuelekea mafanikio na ustawi bora zaidi kutokana na mengi yakiwemo mambo saba ya msingi.

Ananukuu kauli ya Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Nyerere, aliyosema: "Kiongozi bora ni yule ambaye anaaminiwa na wananchi wake. Anapokuwa anaaminiwa, wananchi wake watamtii na kumsaidia kutekeleza malengo."

### Dhamira njema

Mchambuzi Mussa anataja jambo la kwanza linalompaisha Rais Samia kuwa ni uaminifu na dhamira thabiti ya kulitumikia taifa. Anafafanua kwamba Rais Samia ni kiongozi ambaye ahadi zake zimekuwa ni za kuaminika sambamba na vitendo vyake.

"Rais ameonesha dhamira ya dhati ya kuboresha maisha ya Watanzania" anasema mchambuzi huyo.

Anasema hata Rais wa Marekani, Joe Biden, katika hotuba yake ya Desemba 2022 alimsifu Dk Samia kwa uaminifu aliposema, "Rais Samia ni kiongozi mwenye uaminifu usiopingika kutokana na ahadi zake na vitendo vyake."

Anasema Rais Samia ameonesha uaminifu kwa kutekeleza ahadi nyingi, ikiwa ni pamoja na kukuza demokrasia, kuboresha uhuru wa vyombo vya habari na kuongezea bajeti katika maeneo muhimu kama elimu, afya na kilimo.

Anasema ni kutokana na ongezeko la bajeti, sasa miradi mingi inatekelezwa maeneo mbalimbali nchini.

### Uadilifu

Jambo la pili linalosababisha wengi wamwamini Rais Samia, Mussa anasema ni uadilifu wake wa hali ya juu.

Kitabu cha 'The Ethics of Leadership' kilichoandikwa na Warren Bennis na Burt Nanus kinasema: "Kiongozi bora ni mtu ambaye anaamini katika maadili ya jumla na anaishi kulingana na maadili hayo. Kiongozi bora pia ni mtu ambaye anaonesha uaminifu, uwazi, na uadilifu."

Ni katika muktadha huo, mchambuzi anasema Samia ameonesha uadilifu mkubwa katika uongozi wake na kufanya Watanzania wengi kumwamini.

Ananukuu hotuba Rais wa kwanza Mzalendo wa Afrika Kusini huru, Nelson Mandela aliyohusu 'Uadilifu katika Uongozi' aliyoitoa katika Chuo Kikuu cha Yale cha New Haven, Connecticut, Marekani, mwaka 1995 akisema: "Uadilifu ni sifa muhimu zaidi ya kiongozi. Kiongozi mwadilifu ni mtu ambaye anaamini katika maadili ya jumla na anaishi kulingana na maadili hayo."

Mussa anasema Rais Samia ni mfano wa kiongozi mwadilifu na kwamba anafanya kazi kwa unyenyekevu na heshima kwa wananchi wake.

Anasema Rais ameonesha kujitolea katika kupambana na rushwa na ufisadi, na kwamba ameunda Tume ya Maadili ya Viongozi wa Umma na anaendelea kukemea na kuchukua hatua kali dhidi ya watuhumiwa.

Amekuwa pia akionesha uadilifu kwa kuhimiza 'matendo makali' na si 'maneno makali' huku akizungumza wasio waadilifu kwa kalamu.

### Ujasiri wa maamuzi

Sababu ya tatu ya Watanzania kuwa na imani na Rais Samia, mchambuzi anasema ni uwezo na ujasiri wa kufanya maamuzi sahihi.

Katika kujenga hoja yake, mchambuzi anaanza na nukuu kutoka katika kitabu cha "The Power of Decision" kilichoandikwa na Napolein Hill inayosema: "Uamuzi ni msingi wa mafanikio. Uamuzi ni ufunguo wa mafanikio."

Mchambuzi Mussa anasema Rais Samia ni kiongozi mwenye ujasiri katika kutoa maamuzi sahihi yanayolenga kuboresha maisha ya watanzania.

Anatoa mfano wa maamuzi hayo kuwa ni pamoja na kuondoa zuio la mikutano ya siasa, kukutana na kuzungumza na viongozi wa vyama vya upinzani, kutoa ajira na kupandisha vyeo watumishi mbalimbali wa umma.

Anakumbusha pia kwamba katika ripoti ya Mwezi Mei, 2023 ya majarida ya Time na Fortune, Rais Samia ameorodheshwa kama mmoja wa viongozi 100 wenye ushawishi mkubwa duniani na hii ni kutokana na ujasiri wake wa kufanya maamuzi, na dhamira yake ya kuipeleka mbele Tanzania kimaendeleo.

### Ushirikishwaji wananchi

Mussa anaeleza sababu ya nne ambayo inawafanya Watanzania wamwamini Rais Samia kuwa ni ushirikishwaji wa wananchi.

Akifafanua hoja hiyo, Mussa anaanza na nukuu Katika kitabu cha 'The 21 Irrefutable Laws of Leadership' kilichoandikwa na John C. Maxwell inayosema: "Hakuna mtu amezaliwa kuwa kiongozi, lakini kila mtu anaweza kujifunza ujuzi na tabia zinazohitajika kuwa kiongozi mzuri. Na moja ya ujuzi muhimu zaidi ni uwezo wa kusikiliza na kuwashirikisha wengine katika kufanya maamuzi."

Anasema Rais Samia ni mnyenyekevu na daima anapenda kusikiliza maoni ya wananchi. Kwa dhati, ameanzisha mfumo wa mawasiliano wa wazi na wananchi ili kupata maoni yao na kushirikisha wananchi katika mchakato wa uamuzi.

Anatoa mfano wa namna alivyoshirikisha wananchi katika mchakato wa kupanga miradi ya maendeleo, kushirikisha wananchi katika ujenzi na uendeshaji wa miradi ya maendeleo na kushirikisha wananchi katika ufuatiliaji na tathmini ya miradi ya maendeleo. Hata hivi karibuni ameshirikisha wananchi katika suala zima la 'Haki Jinai'.

Anatoa mfano mwingine akisema Rais Samia amekutana na wananchi, viongozi wa dini, jamii na makundi mbalimbali wakiwemo vijana, wazee na wanawake kutoka maeneo mbalimbali nchini, na amesikiliza maoni yao kuhusu masuala mbalimbali.

### Mageuzi makubwa

Mwandishi Mussa anataja jambo la tano alilofanya Rais Samia kuwa ni kufanya mageuzi makubwa ya maendeleo kuanzia ngazi ya vitongoji hadi taifa.

Anasema katika kipindi chake kifupi cha kuwa madarakani, Rais Samia amefanya mageuzi makubwa katika nchi ikiwa ni pamoja kupambana na ufisadi na kutetea haki za binadamu.

Mageuzi haya anasema ni pamoja na kuimarisha uchumi wa nchi kupitia hatua za kuvutia uwekezaji, kuboresha mazingira ya biashara na kuongeza uzalishaji wa mazao na bidhaa.

### Kuleta maendeleo

Anataja jambo la sita linalombeba Rais Samia kwa Watanzania kuwa ni kupambana katika kuleta maendeleo yao. Anasema katika kipindi cha uongozi wake kumekuwa na jitihada kubwa za kuleta maendeleo kwa wananchi wa Tanzania kwa kuendeleza na kuanzisha miradi na mipango mbalimbali ya maendeleo kila kona ya nchi.

Miradi ya maendeleo imeanzishwa ili kuboresha upatikanaji wa huduma mbalimbali zikiwemo za afya na elimu katika maeneo ya vijijini. Pia kumekuwa na jitihada za kuongeza uzalishaji katika sekta ya kilimo kinachoajiri Watanzania wengi, hatua ambayo, mbali na kuongeza kipato cha wakulima inaihakikishia nchi usalama wa chakula.

### Kujali wananchi

Mussa anataja jambo la saba ambalo linawavutia Watanzania wengi kumwamini Rais Samia kuwa ni ukaribu na kujali wananchi wote.

Anafafanua kwamba Rais Samia anafahamika kwa kutembelea sehemu mbalimbali za nchi ili kusikiliza moja kwa moja changamoto na mahitaji ya wananchi kama anavyofanya katika ziara zake dsasa hivi mikoa ya Kusini.

Hii imeonesha dhamira yake ya dhati ya kugusa maisha ya kawaida ya Watanzania. Aidha, Rais Samia amejitolea katika kushughulikia masuala ya kijamii na kibinadamu. Rais ameshiriki pia katika shughuli za kusaidia makundi ya watu wenye uhitaji kama vile watoto yatima, wazee na walemavu.

Mchambuzi anasema kwa kujenga uhusiano wa karibu na kujali mahitaji ya wananchi, Rais Samia ameonesha uongozi wenye huruma na unaozingatia maslahi ya kila mmoja.

Anasema mambo hayo saba yanamfanya Rais Samia kuwa kiongozi ambaye Watanzania wana imani na matumaini naye makubwa katika kuwapa maendeleo na ustawi ulio bora.



Paul Mng'ong'o

## KLINIKI YA FIKRA

Simu: 0676055444 Email: mngongopaul@yahoo.com

# Mambo makubwa matano ya kuzingatia kwenye maisha

KAMA ukiyapa nafasi ya pekee na kipaumbele mambo haya matano tunayoyataja hapa, maisha yako yatakuwa ya baraka na amani.

1. Fanya maamuzi ya dhati kuzingatia afya yako.
2. Fanya bidii ya dhati kukuza uchumi wako.
3. Jenga maarifa na ujuzi kila siku.
4. Hakikisha unakuwa na hekima.
5. Mpende na mtegemee Mungu.

**1. KUHUSU-AFYA**

Afya ndiyo mtaji wa maisha yako. Bila afya, mambo yako muda si mrefu yatasimama kutokana na matatizo ya kiafya. Mambo ya msingi kuhusu afya ni:-

A. Ulaji sahihi – Ni vizuri kula vyakula vyenye virutubisho sahihi na kuepuka sumu mbalimbali. Vitu vikubwa vya kuepuka kwenye ulaji ni:-

- Matumizi makubwa ya wanga mwilini
- Matumizi makubwa ya mafuta. (Yanayoganda na Yasiyoganda)
- Matumizi makubwa ya sukari.
- Matumizi ya dawa yasiyo na ushauri wa wataalam.
- Zingatia unywaji wa maji ya kutosha

B. Mtazamo sahihi – Mtazamo sahihi ni mtazamo chanya. Ni vizuri ujifunze kufikiri kwa mtazamo chanya na achana na fikra zinazokuletea maumivu.

C. Kufanya mazoezi - Mazoezi ni jambo muhimu la kuimarisha afya.

D. Kupumzika - Unapaswa kupata muda mzuri na wa kutosha wa kupumzika.

**2. KUHUSU MAFANIKIO KIUCHUMI**

Mafanikio ya kiuchumi ni zao la uamuzi madhubuti wa kuishi kwa kufuata misingi na kanuni sahihi za kiuchumi. Hakuna njia ya mkato zaidi ya hii. Kuna misingi na kanuni kubwa nne za mafanikio kwenye maisha: -

A. Uamuzi thabiti – Njia za mafanikio ni ngumu na mara nyingi zinavunja moyo na kukatisha tamaa.

Njia hizi zinahitaji kujikana na kuachana na mambo mengine, hivyo si kitu rahisi.

B. Mpango thabiti

Ili kufanikiwa, lazima uwe mtu wa kupanga mambo yako na kuyasimamia sawasawa na mpango. Panga kila kitu, mfano: -

- Panga vizuri jambo/mambo ya kufanya
- Tambua makusudi ya msingi ya jambo husika
- Panga rasilimali zako na mgawanyiko wake
- Tambua na upange mahitaji ili kufanikisha
- Panga wahusika wa jambo kwa sifa na uwezo wao
- Weka vipaumbele
- Panga matumizi sahihi ya muda
- Panga muda unaokusudiwa
- Gawanya muda kwenye vipindi vya tathmini
- Panga viashiria vya matokeo kusudiwa
- Tambua maeneo ya uwezekano wa kushindwa na uyapangie mbinu za suluhu n.k.

C. Jitihada

Mafanikio bila kufanya kazi kwa juhudi, ni sawa na kuyaimba tu mafanikio na kamwe mafanikio halisi hayatatokea.

D. Mtandao itakayokusaidia

Ili kufanikiwa kiuchumi lazima uwe na mtandao (uzungukwe) na watu sahihi watakaokusaidia kukua.

E. Bahati/Fursa

Pamoja na yote, njia ya mafanikio inahitaji bahati kwa lugha ya kijamii au fursa kwa lugha ya kiuchumi. Hapa tunazungumzia mambo makubwa matatu: -

- Upate fursa,
- Uzione fursa, na
- Uzitumie fursa kwa usahihi.

**3. KUHUSU MAARIFA NA UJUZI**

Maarifa na ujuzi ni maelezo ya kinadharia na ya vitendo, ukweli au ujuzi ambao tunapata kupitia uzoefu au kwa kujifunza. Maarifa yetu yanaongezeka tunapopata uzoefu zaidi. Ujuzi uliokuzwa vizuri unaweza kutufanya kuwa wataalam katika uwanja fulani. Ujuzi unaweza kujifunza pia.

**4. KUHUSU HEKIMA**

Hekima ni zao la matumizi ya mjumuiko wa elimu sahihi, ufahamu mzuri, ujuzi, maarifa na uzoefu kwenye kutazama na kutathmini mambo.

Mtu anayefikiria kwanza kabla ya kusema au kutenda na akatenda sawasawa, huyo anahesabika mwenye hekima.

Kuna watu wengi wanapata hali hii kwa kutokana na vyanzo mbalimbali kama vile: -

- Mazingira aliyokulia
- Watu wanaomzunguka
- Miongozo au Misingi anayoiamini
- Kutembea maeneo mengi
- Mambo mengi aliyoona au kukutana nayo
- Elimu na uelewa

Hekima ndiyo ulinzi wa mafanikio tunayokuwa tumeyajenga. Matatizo mengi kwenye maisha ni matokeo ya kufanya maamuzi bila ya kutumia hekima.

**5. KUHUSU MUNGU**

Siri kubwa ya watu waliofanikiwa na wengi kuwa imara (thabiti) kwenye maeneo yao (siri ambayo haitajwi sana), ni kumtegemea na kumcha Mungu wao.

Maisha bila Mungu, ni maisha ya utupu yasiyo na mwelekeo.

**HITIMISHO:**

Hakuna uhaba wa maarifa kwenye zama tunazoishi sasa, maarifa yapo tele na yanapatikana kwa urahisi kabisa.

Unaweza kujua chochote unachotaka kujua.

Kinachokosekana ni juhudi kupata maarifa sahihi na kufanyia kazi yale maarifa ambayo mtu unapata.

Kama ungependa kupata ushauri au usimamizi wa karibu katika kuishi mwongozo huu, (unaweza kuwa taasisi binafsi au ya serikali, kikundi cha kijamii, kanisa, umoja, NGO, mtu binafsi n.k.) basi karibu sana, nitashirikiana nawe kwa neema na msaada wa Mungu.

*Karibu tuwasiliane kwa namba 0676055444 au barua pepe mngongopaul@yahoo.com na kwenye mitandao ya kijamii.*

Paul Mng'ong'o
*Your Partner in Growth.*





Na Hamisi Kibari
Mtanzani wa kwanza kushinda Tuzo ya Taifa ya Mwalimu Nyerere ya Uandishi Bunifu

# Niko tayari kwa kifo-1

JOYCE akiwa amejifunga taulo kuanzia juu ya maziwa, alisimama akiwa amekasirika kwenye mlango wa kutoka chumbani. Katikati ya chumba hicho cha gesti, Chris aliendelea kufunga vishikizo vya shati. Joyce alimwangalia kwa jicho la hasira. Chris alimsogelea pale mlangoni akiendelea kufunga vishikizo vya shati.

"Nimesema hapa haondoki mtu," alifoka Joyce kwa sauti ya juu.

"From the beginning sikukuficha kwamba ninaye mke, Joy. Hatonielewa na sina cha kumwambia kama nitalala huku. Ngoja niende, mpenzi."

"Utajijua kama huwezi kumdanganya. Mimi siwezi kubaki humu peke yangu."

Joyce aligeukia mlango. Akachomoa funguo. Akaenda kuketi kitandani akiwa ameshikilia funguo. Chris alimfuata. Akamwinamia.

"Tafadhali Joy, niache niende tutakuwa wote siku nyingine. Hata kesho ukipenda."

"Nimeshakwambia mimi siwezi kwenda nyumbani usiku huu. Hakuna wa kunifungulia mlango na hapa siwezi kubaki peke yangu. Nimekuja huku kwa ajili yako. Au siyo wewe uliyesema tukutane hapa?"

"Sikiliza Joy... Nikilala hapa wala siwezi kufurahia chochote. Halafu itaniletea taabu sana kwa mke wangu. Nakuomba kwa mara nyingine Joyce, ngoja niende. Najua pengine huwezi kuamini lakini hii ni mara yangu ya kwanza kutoka nje ya ndoa yangu, kwa hiyo mke wangu hawezi kunielewa hata kidogo. Kwanza ninajua huko aliko yuko katika mtanzuko mkubwa wa mawazo. Ndio maana nimezima simu."

Chris alishika mfukoni, akahesabu noti takriban 10 za shilingi 10,000 kila moja. Akampa Joyce. Joyce alizipokea. Akavuta pochi yake kwenye meza, akaziweka hizo noti nyekundu. Zilionekana kumlainisha kwani hata pale Chris alipompokonya funguo, Joyce hakuleta matata yoyote.

"Have a good night, dear," alisema Chris na kunyanyuka.

"No, nisubiri tutoke wote. Nataka nikanywe tena nje labda ndipo nitapata usingizi."

Wanatoka.

* * *

Chris aiingia chumbani kwake huku akijisikia vibaya na hasa kwa



kuwa iliku ni mara yake ya kwanza kusaliti ndoa yake aliyoapa kwa viapo vyote kwamba atailinda dawamu. Mkewe, Mama Kenny aliyetoka kumfungulia mlango, aliketi pembeni mwake. Chris alimnyanyua mwanae mdogo, Huba, na kumpakata. Hata yeye alishangaa kuona yuko macho saa saba hiyo usiku.

"Umesema mtoto anasumbuliwa na nini unadhani?"

"Ana homa kali, nimeshamsiponji mara mbili... Lakini naona joto limepungua," alisema Mama Kenny.

Chris alimshika mtoto sehemu za shingo kusikiliza joto. Kweli aligundua amgali na joto.

"Baba Kenny, kwa nini ulifunga simu muda wote?"

"Pale hoteli nilipokuwa na wale rafiki zangu wa madini kulikuwa na makelele mengi. Hata mtu angepiga simu tusingeelewana," alijibu. Mama Kenny alionekana akiwa na kitu moyoni lakini akabaki kimya. Alimgeukia tena mumewe.

"Vipi, tumpeleke mtoto hospitali?"

"Lakini naona joto limepungua. Kama litazidi tena basi tutampeleka hospitali."

"Baba Kenny, hii hali ya kuniacha mpweke na huku tena mtoto anasumbua imeninyima raha sana. Kama haupo siwezi kupata usingizi... Siku nyingine waombe hao rafiki zako mje mfanyie maongezi hapa nyumbani."

"Ok," alijibu Chris akisimama. Akavua nguo na kuvaa za kulalia. Akazima taa yenye mwanga mkali na kuwasha ya rangi yenye rangi hafifu kisha akajitupa kitandani.

* * *

Chris alinyanyuka kwenye meza baada ya kupata kifungua kinywa. Mama Kenny akitokea jikoni aliketi pembeni mwake.

"Hebu kaa kwanza baba Kenny. Kuna mambo ninataka tuongee kidogo," alisema, lakini Chris bado alisimama, uso wake ukionesha mashaka. Bila shaka alihisi kile ambacho mkewe alitaka kusema. Ni kitu alichokitegemea lakini hakujua kama anayo majibu ya kumridhisha.

"Hatuwezi kuongea baadaye usiku... Ninataka niwahi, Mama Kenny."

"Mtu mwenyewe siku hizi unarejea usiku sana, tutaongea saa ngapi? Jana nilitaka tuyaongee usiku uleule uliporejea lakini nikaona nisubiri tu kuche."

"Enhe, unasemaje mke wangu."

"Baba Kenny, hii tabia ya kuchelewa kurudi usiku mbona inazidi kushika kasi? Jana ilikuwa mara ya tatu unatoka ukiahidi utawahi kurudi lakini unarudi muda umekwenda sana. Jana umerejea saa saba na nusu. Vipi?"

"Jana nilikuta kuna muziki. Jamaa zangu wa madini ni wapenzi sana wa muziki. Mazungumzo yetu yamelazimika kuchukua muda mrefu kwa sababu yalikuwa yanakatishwa katishwa. Hata hivyo, niliwaacha wakiendelea kucheza muziki."

"Kwa nini hutaki kuwaleta hapa nyumbani?" akazidi kuhoji mama Kenny.

"Iko siku nitawaleta mama Kenny... Lakini ninajua utakapoanza kuona manufaa ya hawa jamaa dhiki zote za kubaki peke yako ndani zitaisha. Usiwe na wasiwasi, Mama Kenny."

"Hao rafiki zako kama utaendelea kukutana nao mara kwa mara hawatakuambukiza kweli tabia mbaya mume wangu?"

"Inaonekana huwa unaniona kwa wasiwasi, Mama Kenny. Yaani mwaka wa saba tumeishi bado hujanifahamu mumeo. Kweli unanidhania mimi ni limbukeni wa kuigaiga mambo, siyo?"

"Mara nyingi rafiki mwenye tabia fulani mbaya ni rahisi kukuambukiza tabia yake. Mimi hapa wakati unanioa nilionywa sana kuhusu mashoga na ndio maana unaona sina shoga hapa mtaani..."

"Usiwe na wasiwasi nami. Ni suala la muda tu. Mambo yakishaanza kuwa mazuri nitajitenga na hawa jamaa."

* * *

Kulikuwa na watu kadhaa katika hoteli ya kisasa ya Lemon Tree ya mjini Tabora. Katika kona moja aliketi Chris na Joyce. Kama kawaida alichagua kiketi kwenye kona yenye giza kiasi ambayo aliamini si rahisi watu kumfahamu katika manispaa hiyo.

"Wewe mhudumu, njoo hapa," aliita Chris.

Mhudumu alikuja pale mezani. Akasimama kando yao. "Chukua hiyo bia utupelekee chumba kiitwacho Tanga kama hakina mtu, halafu utaleta kinywaji kingine kama hiki."

Chris alimshika mkono Joyce ambaye alikuwa ameanza kulewa dakika chache baada ya yule mhudumu kurejea na kuwaambia kwamba tayari, chumba kinawasubiri.

Mapema kabla ya uamuzi huo wa kwenda chumbani, Chris alikuwa amepanga kurejea mapema nyumbani, lakini kuna jambo lilikuwa limeanza kumchanganya. Alishindwa kukaa zaidi ya siku tatu bila kukutana na Joyce. Na walipokutana, alijikuta akishindwa kuachana na msichana huyu mrembo bila kujifungia naye chumbani! Kuna jambo lingine lilianza kujitokeza pia. Alifurahia zaidi penzi la wizi la msichana huyu ambaye ilionekana amekubuhu katika mambo ya kupumbaza wanaume kulinganisha na mkewe.

Wakati wakati wanaelekea chumbani, Chris alikuwa akijisemea: "Eti wanasema kwa nini umalize bucha wakati nyama ni ileile, si kweli. Nyama nyingine zimenona kuliko nyingine."

Waliingia chumbani, chumba alichozoea kuingia na msichana huyo, huku akiwaza namna ambavyo anazidi kumkasirisha mkewe, Mama Kenny. Alikumbuka tena namna siku hizo alivyokuwa mbali na wanawe wawili wapendwa usiku, Kenny aliyekuwa anasoma darasa la kwanza na Huba ambaye likuwa ana umri wa miaka miwili.

Chris aliketi kitandani, Joyce aliketi kwenye kiti kilichokuwa pembeni chumbani humo. Aliangalia saa, ililekea saa nne usiku.

"Bia si utaendelea kunywa mimi nikitoka? Njoo bwana huku," alisema Chris akimshika mkono Joyce.

Mwanamke huyo alichukua glasi ya bia nusu na kumlazimisha Chris kunywa. Chris alikataa.

"Mambo mawili yamenichosha kwako. Kunywa pombe peke yangu bila wewe kuniunga mkono na pili kuniacha humu chumbani nikilala peke yangu."

Chris hakujibu kitu bali alisimama na kuvua shati lake, kisha suruali na kutundika kwenye henga, chumbani humo. Alitaka wamalize shughuli iliyowaingiza hapo chumbani awahi kuondoka.

Joye alinyanyuka na kwenda maliwatoni kujisaidia haja ndogo. Alipotoka huko alimkuta Chris akiwa amejilaza kitandani. Alisimama pale katikati ya chumba kisha akapata wazo. Akaanua nguo za Chris na kuingia nazo chooni. Akazibwaga ndani ya ndoo ya maji. Chris alishutuka na kumfuata mlangoni mwa choo hiyo ndani ya chumba hicho.

"Leo hak'ya Mungu huniachi humu peke yangu. Lazima tulale wote mpaka asubuhi na hii ndio namna ya kukukomesha. Yaani inaonekana mkeo unamjali sana kuliko mimi," alisema Joyce.

"Joyce, umefanya nini sasa?" Alimaka Chris huku akiangalia nguo zake zikiendelea kuzama ndani ya maji.

***Itaendelea wiki ijayo***

# Mackenzie, wenzake 29 kuzidi kusota rumande

**NAIROBI, Kenya**



KATIKA hali isiyo ya kawaida, hakuna kesi iliyosikilizwa juzi katika Mahakama za Sheria za Shanzu katika kesi inayomkabili Mchungaji Mackenzie na washtakiwa wenzake 29.

Badala yake upande wa Jamhuri uliwasilisha ombi la kutaka Mackenzie na wenzake wazuiliwe kwa siku 180 mahabusu ili kupisha upelelezi kuendelea.

Mahakama ilipiga kalenda kesi hiyo hadi Oktoba 12, mwaka huu itakapokuja tena mahakamani kwa hatua nyingine.

Uamuzi huu unaonesha kwamba Mackenzie na wenzake, wataendelea kusota mahabusu huku taratibu za kisheria zikiendelea kukamilishwa.

Wakili wa utetezi, Wycliffe Makasembo, alisema hajajiandaa kwa ajili ya kusikilizwa kwa kesi hiyo na kwamba bado wahusika hawajapokea maombi kwa ajili hiyo.

Hata hivyo, ripoti ya idara inayochunguza hali ya washtakiwa haikuwa tayari kutoa maelezo ya kina wakati huo. VOA.

# Uhaba wa majiwawakimbiza tembo Zimbabwe



**HARARE, Zimbabwe**

MAKUNDI makubwa ya tembo wanaihama hifadhi kubwa ya wanyama pori nchini Zimbabwe na kuingia taifa jirani la Botswana wakitafuta maji, hali inayotishia kuongezeka kwa makabiliano kati ya watu na wanyamapori.

Hayo yameelezwa na msemaji wa Mamlaka ya Hifadhi za Taifa za Zimbabwe, Tinashe Farawo, akifafanua kwamba tembo hao walianza kuhama tangu Agosti mwaka huu na kwamba wanaelekea nchini Botswana baada ya vyanzo vya maji kukauka kwenye mbuga ya wanyama ya Hwange nchini humo.

Inaaminika sababu za kukauka kwa vyanzo vya maji ni athari za mabadiliko ya tabianchi na shughuli za mwanadamu.

Farawo amesema idadi ya tembo wanaohama ni kubwa na hofu iliyoko ni kwamba watalazimika kupita kwenye maeneo yenye shughuli nyingi za binadamu.

Mwaka jana pekee tembo walisababisha vifo vya watu 60 na takwimu zinaonesha uwepo wa ongezeko la mwingiliano baina ya watu na wanyama hao wa mwituni.



# Waandamana uwajibikaji duni kwenye mafuriko

**TRIPOLI, Libya**

MAMIA ya watu waliandamana Jumatano iliyopita katika mji wa mashariki mwa Libya wa Derna, kuelezea ghadhabu yao kwa kile walichodai ni mamlaka kukosa uwajibikaji, wiki moja baada ya mafuriko yaliyoua maelfu ya wakazi wake na kusababisha uharibifu mkubwa.

Waandamanaji hao walilenga maafisa, akiwemo Mkuu wa Bunge la Libya Aguila Saleh lenye makao yake mashariki mwa nchi, walipokusanyika nje ya Msikiti wa Sahaba.

Wengine waliketi juu ya paa la jengo la bunge, kwa mujibu wa vyombo vya habari.

Waandamanaji hao wenye hasira walichoma moto nyumba ya aliyekuwa meya wa mji wa Derna wakati wa mafuriko hayo, Abdulmenam al-Ghaithi, meneja wa ofisi yake aliviambia vyombo vya habari.

Waandamanaji hao walidai kama kungekuwa na uwejibaki mzuri mafuriko yasingetokea na kwamba hata baada ya kutokea, athari zake zisingekuwa kubwa.

*VOA*

# Wizi waifanya EU kusitisha ufadhili wa chakula Somalia

**MOGADISHU, Somalia**

UMOJA wa Ulaya (EU), umesitisha kwa muda ufadhili wake kwa Shirika la Mpango wa Chakula Duniani (WFP) nchini Somalia kwa kile kilichoelezwa kuwa ni kutokana na wizi na utumiaji mbaya wa misaada.

Hayo ni kwa mujibu wa maofisa wawili wakuu wa EU waliozungumza na Shirika la Habari la Reuters Jumatatu iliyopita baada ya uchunguzi kubaini wizi mkubwa na matumizi mabaya ya misaada ambayo ilikuwa na lengo la kuepusha baa la njaa.

Tume ya Ulaya ilitoa msaada wa zaidi ya Dola za Marekani milioni 7 kwa operesheni za WFP nchini Somalia mwaka jana, ikiwa ni sehemu ya zaidi ya dola bilioni moja ilizopokea katika michango yote, kulingana na takwimu za Umoja wa Mataifa. Nchi wanachama wa EU zilitoa pesa nyingi zaidi, kwa misingi ya ushirikiano wa nchi kwa nchi.

Haikubainika mara moja kama kuna nchi nyingine binafsi ambazo zingeungana na EU kusitisha misaada. Msemaji wa Tume ya Ulaya, Balazs Ujvari, hakuthibitisha wala kukanusha moja kwa moja taarifa za kusimamishwa kwa misaada kwa muda.

Hata hivyo, alisema: "Hadi sasa, EU haijafahamishwa na washirika wake wa Umoja wa Mataifa kuhusu athari za kifedha kwa miradi inayofadhiliwa na muungano huo."

WFP haikujibu mara moja maombi ya Reuters ya kutaka itoe kauli kuhusu suala hilo.

*VOA*

# Mapigano yasambaa Sudan



**KHARTOUM, Sudan**

MAPIGANO kati ya pande mbili zinazohasimiana za Jeshi la Sudan yameenea hadi mji wa Port Sudan kwa mara ya kwanza katika kipindi cha miezi mitano ya vita.

Wanajeshi wa Sudan walifyatuliana risasi na wanachama wa kundi la wanamgambo wa kabila linalojiita Forces of the Eastern Sudan Parties and Movements Alliance.

Wanajeshi hao walijaribu kuondoa vizuizi vilivyowekwa na kundi hilo juzi katikati ya jiji hilo.

Bandari ya Sudan ni mwenyeji wa uwanja wa ndege pekee unaofanya kazi nchini humo.

Mji huo pia ni mahali ambapo baadhi ya maofisa wa serikali na mashirika ya Umoja wa Mataifa wamehamia kutokana na mapigano katika mji mkuu, Khartoum na kwingineko nchini humo.

Mapigano kati ya jeshi la Sudan na Vikosi hasimu vya Wanajeshi wa Msaada wa Haraka RSF, yamesababisha maelfu ya watu kuuawa tangu ghasia kuzuka katika mji mkuu, Khartoum, mwezi Aprili.

*BBC*

# Dk. Mpango awasili Marekani



**Na Mwandishi Wetu, Marekani**

MAKAMU wa Rais, Dk. Phillip Mpango amewasili nchini Marekani kumwakilisha Rais Dk. Samia Suluhu Hassan katika Mkutano wa Baraza Kuu la 78 la Umoja wa Mataifa (UNGS78).

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa kwa vyombo vya habari na Msaidizi wa Makamu wa Rais, Habari, Franco Singaile, Dk. Mpango ataongoza ujumbe wa Tanzania katika mikutano mbalimbali.

Makamu wa Rais ataongoza mikutano, inayohusu mazingira, uchumi, afya, maji, demokrasia na Malengo ya Maendeleo Endelevu ambayo Tanzania imealikwa na nchi washirika, taasisi za kimataifa na Asasi binafsi.

Aidha, anatarajia kuhutubia Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa katika ukumbi wa mikutano jijini New York Marekani, Septemba 21, mwaka huu.

# Sasa Robertinho amekuwa hafai?

**Na Ibrahim Mkamba**



> **Chama kapunguza nguvu kampeni ya ondoa Robertinho, leta Mgunda. Kampeni hiyo ingekuwa nzuri zaidi Simba wangelala. Chama kaharibu mpango. Ni wazi Robertinho akiondolewa nafasi yake ataikaimu Mgunda. Je atafanya kila jambo zuri tupu?**

TANGU Simba itoke sare ya 2-2 na Power Dynamo ugenini, post za ubovu wa Simba na ubovu wa kocha Robertinho zimekuwa nyingi mno. Zaidi zinatokana na utaratibu wetu wa kuishi maisha ya kufuata mkumbo.

Watu wamechachamaa kuwasema vibaya wachezaji na kocha wa Simba utadhani mechi ya Power Dynamo na Simba ugenini ilikuwa kati ya Simba na Ngome ya Temeke iliyochezwa Dar! Angalau Clatous Chama amesifiwasifiwa.

Je hakuna wachezaji zaidi ya Clatous Chama wa kusifiwa? Je ni halali watu kuponda tu bila hata kuona ya kusifu? Vipi assist ya Miquissone ya goli la pili la kusawazisha, haikustahili kusifiwa? Kiki ya Mzamiru iliyotemwa kusababisha goli la kusawazisha si jambo la kusifiwa?

Nionavyo hata sare hiyo ya ugenini ilistahili pongezi ikizingatiwa hii imekuwa sare ya kwanza ya Simba Zambia kwenye mashindano ya Afrika miaka hii. Mechi zote huko ilikuwa inalala.

Post zote za matokeo ya Yanga dhidi ya El Merreikh zinavutia mno kuzisoma kwani zimejaa sifa kwa wachezaji na kocha wakipambwa sana tena sana. Ni kauli zinazoleta raha na hamasa kubwa kwa timu kwa mechi ya marudiano. Hii wala haitokani na ushindi bali inatokana na upendo kwani hata Simba walivyozishinda Mtibwa Sugar na Dodoma Jiji kauli za "hatuna kocha" zilikuwepo.

Watu kadhaa wa Simba wanaona raha Simba kutopata ushindi ili wapate fursa ya kuwasema vibaya wachezaji na kocha wao. Je Simba wakifanya vizuri hao jamaa watakuwa na nini cha kuandika? Ukweli post hizo zinaboa kwani ni nyingi na zimekuwa monotonous mno.

Kama kuna watu wangetilia maanani hoja hizo, naona wazi watazipuuza kwa kuziona kama ni mkakati maalum kwa jinsi zilivyo monotonous. Inakera.



Kwa mjadala unaoendelea sasa wa toa Robertinho, leta Juma Mgunda, ingefaa sana Simba ife 2-1 nyumbani kwa Power Dynamo ili kampeni ya toa Robertinho, leta Mgunda iwe nzuri.

Kuna watu wa Simba wanamchukia sana Robertinho kwa mabaya mengi wanayomuorodheshea yanayozima hali ya yeye kuwa hajapoteza mechi nyingi tangu afike Simba.

Ukweli wa wazi ni kwamba kocha huyo hatakiwi kabisa na baadhi ya watu wa Simba. Naamini siku akiondoka kuna watu watu wanaoishabikia Simba watafanya sherehe bila kujali atakuwa amewafanikishia makubwa yapi.

Kitu ambacho wengi wanasahau ni kwamba tangu Simba ianze utaratibu wa kuingia makundi mashindano ya Afrika, haijawahi kupata sare Zambia, hii ikiwa sare yao ya kwanza. Kule wao ni kupigwa tu.

Walifungwa 2-1 Zambia na Nkana Red Devils kisha wakashinda Dar 3-1 wakaingia makundi. Waliishinda Red Arrors 3-0 Tanzania na kulala 2-1 Zambia. Sasa kwa mara ya kwanza wamepata sare Zambia miaka hii na kelele ni hizi. Hata sijui wangeshindwa kama kawaida yao ingekuwaje!

Chama kapunguza nguvu kampeni ya ondoa Robertinho, leta Mgunda. Kampeni hiyo ingekuwa nzuri zaidi Simba wangelala. Chama kaharibu mpango. Ni wazi Robertinho akiondolewa nafasi yake ataikaimu Mgunda. Je atafanya kila jambo zuri tupu?

Je wanaomuunga mkono Robertinho sasa hivi, hawatakuwa wakimnyanyasa Mgunda kila akikosa matokeo mazuri? Usishangae pia kukuta wanaopiga kelele sasa kumtaka Mgunda, watamgeuka.



Nakumbuka Mgunda alimpiga Geita Gold 0-5 Mwanza. "Hakuna kocha kama huyu." Alisema jamaa yangu mmoja na wenzake.

Akaenda Bukoba akakamatwa kwa sare na Kagera Sugar. Nasisitiza sare si kushindwa. "Mgunda si kocha, anababatisha. Aondoke." Akasema jamaa yangu yule yule ndani ya muda mfupi hivyo! Tunachosahau ni kwamba kila timu huhitaji matokeo mazuri.

Tazama matokeo ya mechi zilizokwishachezwa za ligi ya mabingwa Afrika; Bumamuru 0-4 Mamelody Sundown, ES Sahel 1-0 AS FAR, Real Bamako 0-3 Nouadhibou ya Mauritania, El Merreikh 0-2 Young Africans, Power Dynamo 2-2 Simba. Mechi nyingi leo.

# Wananchi wa Nje ya Uwanja walienda kufanya nini Kigali?



**Na Mwandishi Wetu**

SIKUTAZAMA maonesho ya moja kwa moja ya mechi za ugenini za Yanga Kigali na Simba Ndola. Nimetazama marudio ya mechi ya El Merreikh na Yanga na kuona mambo ambayo siku hizi hayasemwi kuhusu Yanga kwani sasa hivi tumeamua kuwasifu tu Yanga jambo ambalo haliwasaidii.

Nimeona tofauti kiuwezo kati ya El Merreikh na Yanga ni kubwa sana ambapo Yanga walikuwa juu kwa umbali mrefu kiuwezo. Hii haina maana El Merreikh ni timu mbovu. La hasha. Hii inatokana na kupanda uwezo kwa Yanga kulikowafanya wacheze kwa kurelax mno.

El Merreikh si wabovu kwani walipambana sana hasa baada ya kufungwa magoli yote mawili. Aidha, hao waliwatoa mashindanoni mabingwa wa Congo Brazaville na pia wana wachezaji wengi kwenye timu ya taifa ya Sudan. Si wabovu bali walizidiwa uwezo.

Paccome alikuwa anayachukulia mambo ya uwanjani kama madogo na rahisi sana. Nahitaji sana kumuona kijana huyu mwenye akili nyingi ya soka atakapocheza kikweli kweli Yanga itakapokutana na timu kubwa za bara hili.

Goli la kwanza lililoanzia kwenye free kick ya Paccome na kumalizwa kwa kichwa na Musonda lilivutia mno na wazi hiyo ni kazi ya mazoezini. Hata la Mzize la pasi ya kisigino ya Azizi Ki nalo ni la kazi ya mazoezini. Pamoja na mazuri mengi ya Yanga, wengine hawawaambii upungufu wao kadhaa bali mimi nitawaambia Yanga kwa faida yao ya siku zijazo.

Kwanza, licha kubaini upungufu kadhaa wa El Merreikh, Yanga hawakuwa wakali (hawakuwa aggressive) kuliandama lango la wapinzani wao hao. Muda mrefu waliutumia kuburudisha tu.

Pili, nimeona mara kadhaa walizofika eneo la lango la El Merreikh walikosa utulivu kwenye kufunga. Wanapaswa wabadilike kwa hayo mawili huko kugumu waendako nikiamini hapa wameshavuka ingawa soka ina maajabu.

Tatu, kwenye ulinzi walitoa 'ruhusa' nyingi za kukoswakoswa; free headers, kipa Diarra kuruka kwa 'timing' ya kukosewa na kuwaruhusu El Merreikh waje sana golini kwa Yanga baada ya goli la pili. Hayo hayafai huko mbele ya safari kwenye matimu makubwa ya Afrika.

Niliyoyaona ndani ya uwanja ya kufanyiwa marekebisho ni hayo. Kwa nje ya uwanja nimejiuliza wenzetu waliosafiri mpaka Kigali walienda kufanya nini? Walijaa upande mmoja wote wa uwanja lakini walikuwa HAWASHANGILII wakisubiri kushangilia magoli tu!

Ukiondoa waliokuwa wakitembea tembea jukwaani na milio ya ngoma na tarumbeta, wengine walikuwa wanaonekana kama picha ya mnato kwa jinsi walivyotulia! Kulikuwa na haja gani kuwemo uwanjani na kutazama mpira kama uko kwenye kibanda umiza? Unaenda uwanjani zaidi kwa kushangilia hasa usafiripo na timu kwenda nchi za watu.

Ipo haja kabla ya kusafiri na timu kwenda nje ya nchi, washangiliaji wahamasishane kwenda kushangilia. Wingi wao wala haukuwatisha El Merreikh kwani hakukuwa na oya oya ya nguvu iliyolingana na wingi wa Wananchi wa njano na kijani walioupamba uwanja. Turekebishe hilo ugenini na nyumbani.

Timu zetu zote zipambwe bila kuacha kuelezwa upungufu wao hasa na watu wenye utaalam wa soka ya uwanjani. Kufanya hivyo si kuwashusha hadhi kwani hakuna timu duniani isiyokosea. Kufanya hivyo ni kuwasaidia wawe bora zaidi.





# Guardiola awataka City kufanya kweli

**LONDON, England**

KOCHA Pep Guardiola anasema Manchester City haijafanya chochote maalum baada ya kushinda Ligi ya Mabingwa mara moja tu.

Kwa kauli hiyo, Pep anataka kikosi chake ambacho kimepotezs taji la ngao ya jamii, kuhakikisha wanatetea mataji yaliyobaki na kuongeza makombe mengine.

City wataanza kutetea taji lao la Ligi ya Mabingwa watakapomenyana na Red Star Belgrade nyumbani Jumanne.

“Itakuwa rahisi zaidi. Kigumu zaidi kushinda ni cha kwanza,” Guardiola alisema.

“Kwa klabu yetu kushinda Ligi ya Mabingwa si ajabu, lakini kwa mtazamo, ni wangapi walioshinda Ligi ya Mabingwa mara moja?

Beki wa Uingereza Kyle Walker alisema City ambao ni vinara wa Ligi Kuu ya England wakiwa na ushindi mara tano kati ya tano, hawatazingatia mafanikio ya Ligi ya Mabingwa msimu uliopita.”

Tulichofanya ni kipindi cha nyuma sasa, ni msimu mpya. Meneja alichora mchoro na kutuweka chini ya mlima na lazima tupande tena,” alisema Walker, ambaye alisaini mkataba wa nyongeza na City. Wiki iliyopita.

Pamoja na Red Star Belgrade ya Serbia, City wameunganishwa katika Ligi ya Mabingwa Kundi G na klabu ya RB Leipzig ya Ujerumani na Young Boys ya Uswizi.

# United kuwakosa sita dhidI ya Bayern

**London , UINGEREZA**




HABARI kwamba Aaron Wan-Bissaka atakuwa nje kwa idadi ya wiki kadhaa kutokana na jeraha zilizidisha hali mbaya kwa mkufunzi wa Manchester United Erik ten Hag.

Wan Bissaka anaungana na Raphael Varane, Luke Shaw, Tyrrell Malacia, Amad na Kobbie Mainoo kwenye orodha ya majeruhi wa muda mrefu.

Wachezaji wapya Mason Mount na Sofyan Amrabat pia walikosa kichapo cha Jumamosi kutoka kwa Brighton kutokana na jeraha, huku Jadon Sancho na Antony wakiondolewa kwa sababu za nje ya uwanja.

United wamepoteza michezo mitatu kati ya mitano. Wanarejea kwenye kibarua cha Ligi ya Mabingwa ugenini dhidi ya Bayern Munich kesho.

United Wameweka kikao cha mafunzo huko Carrington kwa ajilo ya kujifua zaidi. Ni kijivu na mvua kuhakikisha wanapata matokeo dhidi ya bayern japo hawakuanza vizur msimu wao na wachezaji wao wengi tegemezi kutokuwa na kiwango kizuri na kusumbuliwa na majeraha.

# UEFA bila Messi wala Ronaldo





**LONDON, England**

ILE ndoto ya kuwaona Cristiano Ronaldo na Lionel Messi kwenye hatua kubwa zaidi ya kandanda ya Ulaya yalitolewa, lakini hakuna hata mmoja atakayeshiriki Ligi ya Mabingwa msimu huu.

Ronaldo alikuwa mmoja wa watu wa kwanza wenye majina makubwa kuhamia Saudi Arabia - anachezea Al Nassr - wakati Messi yuko Marekani na Inter Miami.

Sio wawili pekee waliokosekana, mshambuliaji wa Brazil Neymar na mshambuliaji wa Ufaransa, Karim Benzema wamejiunga na Ronaldo kwenye Ligi ya Saudia.

Bado tutaona baadhi ya majina makubwa ya sasa na yajayo, huku mshambuliaji wa Ufaransa Kylian Mbappe akiwa PSG na mtambo wa mabao wa City Erling Haaland akitafuta kuvunja rekodi zaidi.

Lamine Yamal mwenye umri wa miaka 16 mwaka huu alikua mchezaji mdogo zaidi wa Barcelona wakati wote na pia mchezaji wa kwanza na mfungaji wa kwanza wa Uhispania

# Mzungu Singida FG amwaga mboga

**Na Mwandishi Wetu**



PALE Singida ni kama hapakaliki sawasawa, siku chache baada ya Ernst Middendorp kuchukua mikoba ya Mzee Vans Pluijms, Kocha huyo mpya amebwaga manyanga.

Wakati taarifa zake jana zikisambaa kwa kasi juu ya kujiondoa kwake, uongozi wa Singida uliibuka na kueleza Kocha ana matatizo ya kifamilia lakini atarudi akimaliza changamoto.

"Tumuombee Kocha amalize changamoto zake haraka," alisema Ofisa Uhusiano wa Singida, Hussein Massanza.

Ni kweli kocha wetu Ernst ameondoka kwa dharura lakini sio kwa sababu zinazotajwa. Kocha na yeye ni binadamu kuna changamoto zake binafsi anapitia so ameenda kuzitatua," alisema.

Mapema asubuhi taarifa zilisema kumetokea kutokuelewana baina ya Mmiliki wa timu hiyo na Kocha huyo ambaye hana zaidi ya mwezi tangu ajiunge na kikosi hicho.

Majira ya tisa taarifa ya Kocha ilisema ameamua kuondoka Singida kutokana na kuingiliwa majukumu yake ikiwa ni pamoja na kupangiwa wachezaji wapi waanze wapi wawe benchi.

"Hili kwangu ni jambo ambalo siliafiki, nimefanya mazoezi na wachezaji, tumepata ushindi kwa timu ngumu kama Future, mimi nilidhani tungepongezwa uongozi unalalamika mabao hayatoshi,

Ernst alijiunga na Singida kuchukua nafasi ya Hans ambaye aliamua kujiengua katika timu hiyo baada ya kuhitilifiana na uongozi wa timu hiyo mara baada ya mchezo wa ngao ya Jamii dhidi ya Azam.

"Ningeshauri tumpe nafasi na tumuombee azimalize mapema ili arejee kwenye majukumu yake. Mwarabu bado hatujamalizana nae," alisema. Kauli nyingine iliyotolewa na Singida bila kujua Kocha huyo ameshamwaga mboga.

Singida ina kibarua kigumu wiki moja ijayo itakapopambana na Future ya Misri katika mashindano ya Kombe la Shirikisho Barani Afrika. Katika mechi ya kwanza, Singida walishinda kwa bao 1-0 hivyo kuhitaji ushindi ama sare yoyote kuweza kusonga mbele.

# LUPASO yaendelea kusukwa



**Na Mwandishi Wetu**

BAADA ya ziara za kustukiza kwenye Uwanja wa Benjamini Mkapa, Dar es Salaam mambo yameonekana kuboreka katika ukarabati wa unaoendelea kuelekea michuano ya CAF Super League.

Juzi jioni nyayaa zote zinapoleka umeme katika Uwanja huo zimeondolewa na kuanza kusukwa upya katika kuhakikisha mechi zinaweza kuchezwa wakati wote.

Wiki iliyopita Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo, Dk. Damas Ndumbaro aliwataka wakandarasi wanaofanya matengenezo ya Uwanja huo kuhakikisha wanamaliza kila kitu kinachohusika na michuano ya CAF Super League kabla ya tarehe 15.

Siku chache baadae Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Said Yakub alitembelea tena uwanja huo na kumtaka mkandarasi huyo sasa kufanya kazi saa 24 ili kila kitu kikamilike kwa wakati.

Katika michuano hiyo, Simba itawakilisha Tanzania huku, timu za Enyimba ya Nigeria, Petro Atletico ya Angola, TP Mazembe ya Congo, Al Ahly ya Misri, Mamelod Sundown ya Afrika Kusini, Wydad Cassablanca ya Morocco na Esperence ya Tunisia.

# Serikali yataka Gofu kwa vijana

**Mwandishi Wetu, Arusha**



SERIKALI imeutaka uongozi wa Chama cha Gofu wanawake (TLGU) umetakiwa kuwekeza zaidi katika wachezaji wa Gofu Vijana ili kupata wachezaji wapya watakaoleta chachu na ushindani zaidi katika mchezo huo pamoja na kupata wachezaji wazuri watakaounda timu ya Taifa.

Ofisa Michezo wa Baraza la Michezo la Taifa (BMT), Halima Bushiri ametoa kauli hiyo wakati wa ufungaji wa mashindano ya Gofu wanawake 2023 yaliyofanyika katika viwanja vya Kiligolf Estate Mkoani Arusha.

"kwanza kabisa niwapongeze sana viongozi kwa kuandaa mashindano haya vizuri kabisa, lakini pia wadhamini mliojitokeza nawashukuru sana kwa kuunga mkono jitihada za Serikali kwa kuendeleza michezo yetu hapa nchini," alisema.

Katika mashindano hayo yaliyofanyika kwa siku tatu katika mikoa ya Arusha na Kilimanjaro, Mtanzania Vicky Elias alitwaa ubingwa wa michuano hiyo.

Huku Madina Iddi wa Tanzania akishika nafasi ya pili na Wakenya Mercy Nyanchama na Ashley Awuor wakishika nafasi ya tatu na nne.

Leo yetu ndiyo kesho yetu
Uelekeo Spoti
| Jumatano Septemba 20 - 26, 2023|

## UEFA bila Messi wala Ronaldo








# Yanga kurejea mahala pake leo?

**Na Mwandishi Wetu**

MABINGWA wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Yanga ya Dar es Salaam leo wanarudi kwenye michuano ya ndani, na leo swali kubwa je, wanarudi mahala pao?

Ni Katika mechi ya mzunguko wa Ligi hiyo ambapo Yanga wanawakaribisgha Namungo pale Chamazi Complex, saa moja kamili usiku.

Uko shindano wa aina Fulani ambao leo utaonekana pale, hasa kutokana na Kocha Mkuu wa Namungo, Cedric Kaze kuwahi kuwahi kuinoa Yanga kama kocha mkuu na baadae kuwa kocha msaidizi chini ya Nasredine Nabi.

Katika mechi mbili, Yanga wamefunga mabao kumi, ushindi ambao ulibezwa na Kaze aliyesema yeye anachoangalia ni ushindi sio idadi ya magoli ya kufunga.

Lakini kimsingi inaonekana sasa ili timu zingine ziweze kukalia kiti cha ligi hiyo ni kuhakikisha Yanga haichezi. Mashujaa wamekalia kiti hicho kwa siku tatu ambapo Yanga wamekuwa kwenye majukumu ya kimataifa.

Yanga inareje katika ligi ikiwa imetoka kumpiga El Marreikh ya Sudan mabao 2-0 katika michuano ya Klabu Barani Afrika pambano ambalo lilifanyika mjini Kigali, Rwanda.

Katika mechi ya leo, Yanga watasimama kwa dakika moja katika dakika ya 12 kutoa shukrani kwa mashabiki walioisapoti timu hiyo katika pambano hilo la Rwanda.


Kwa upande wake Kaze, amesema anajua anacheza na timu bora na ametengeneza plani yake kuhakikisha wanapata matiokeo mazuri katika mechi ya leo.



## Guardiola awataka City kufanya kweli

Uk. 22

## Serikali yataka Gofu kwa vijana



Uk. 23



## Mzungu Singida amwaga mboga

Uk. 23